




**Mchakato** mbunge kupandishwa kizimbani waiva, naye anena

UKURASA 4


BUFE
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
Tumetimiza kivitendo agizo la Majaliwa, kubuni mbegu ya zabibu yenye tija kitaifa
UCHUMI
SAFARI YA MAENDELEO AWAMU SITA
Simulizi Rais Dk. Samia anavyosimamia mageuzi kwenye PPP na uwekezaji wake

UKURASA 11


# Nipashe

Ijumaa Agosti 25, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581413 www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



Askofu Dk. Fredrick Shoo

# Zilivyo mbivu, mbichi kumpata Mkuu wa KKKT

UKURASA 2


Askofu Dk. Benson Bagonza


Askofu Dk. George Fihavango


Askofu Dk. Blaston Gaville


Askofu Dk. Abednego Keshomshahara

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### WATUMISHI TANESCO WASOMEWA MASHTAKA 125

WATUMISHI wawili wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Wilaya ya Nyamagana...

UKURASA WA 4

### CMSA YABARIKI CRDB KUTOA HATIFUNGANI YA KIJANI

KATIKA kuongeza uwezo wake wa kufanya uwezeshaji wa miradi rafiki kwa mazingira...



UKURASA WA 19

### NANI ANAHUSIKA KIFO CHA BOSI WAGNER?

DUNIA imepigwa na butwaa baada ya kiongozi wa kundi la...

# JWTZ kuendesha msako sare zake baada ya wiki

UKURASA 8



# Waagizaji mafuta wakwama kisa Dola

UKURASA 3

**MICHEZO** YANGA SC YAHAMISHIA MAJESHI CAF UK.24

**KATUNI** UK.6




Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa kwenye mazungumzo na Rais wa China, Xi Jinping kando ya Mkutano wa BRICS unaofanyika Jijini Johannesburg nchini Afrika Kusini jana. **PICHA: IKULU**

# Zilivyo mbivu, mbichi kumpata Mkuu KKKT

**Na Waandishi Wetu,** ARUSHA

SHUGHULI ya kumsaka mrithi wa Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Frederick Shoo ni pevu, baada ya wajumbe wa mkutano mkuu wa 21 wa kanisa hilo, kukesha wakikuna vichwa kumpata kiongozi mpya wa sita wa taasisi hiyo.

Hadi kufikia saa 2.10 usiku jana, majina ya wagombea wa kiti hicho yalikuwa bado hayajatangazwa na maaskofu wa Dayosisi 27 za KKKT na wajumbe wengine wa uchaguzi huo walikuwa wamejifungia, licha ya ratiba kuonyesha uchaguzi huo ungefanyika kuanzia saa 10:00 jioni

Kabla ya kuanza, uchaguzi huo uligubikwa na hekaheka za kupigana vikumbo kwa wajumbe wengine kutafuta kura za 'mpendwa' wao wanayemtaka kubeba mikoba ya Dk. Shoo anayemaliza muda wake baada ya kuongoza kwa vipindi viwili.

Agosti 23, 2019, Askofu Dk. Shoo wa Dayosisi ya Kaskazini, alichaguliwa kwa kipindi cha pili kuiongoza KKKT kwa kipindi cha miaka minne. Aliibuka mshindi kwa kupata kura 144 kati ya 218 zilizopigwa katika kinyang'anyiro hicho, akimwacha mbali

mpinzani wake, Askofu Dk. Abednego Keshomshahara wa Dayosisi ya Kaskazini Magharibi aliyeambulia kura 74.

**HALI YA JANA**

Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa 21 wa KKKT, ulioanza Agosti 20 na kutamatika leo katika Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira, Usa River, Arusha, walikuwa wamekusanyika makundi makundi nje ya ukumbi kabla ya kuanza uchaguzi huo, huku usiri ukitawala kuhusu majina ya waliopitishwa kugombea kiti hicho.

Awali, maaskofu hao na wajumbe wengine wa mkutano mkuu, walitanguliwa na ajenda muhimu ikiwamo taarifa ya mambo toka Halmashauri Kuu, ikafuatiwa na ajenda ya vikundi vya majadiliano, Halmashauri Kuu ya Kanisa kisha uchaguzi.

Kabla ya kuanza kwa uchaguzi huo, kulikuwa na taarifa kutoka ndani kwamba majina ya maaskofu watatu yalikuwa yanatajwa kuwa na ushawishi mkubwa kwenye kinyang'anyiro cha nafasi hiyo.

Maaskofu waliokuwa wakitajwa kuwa wamependekezwa katika kinyang'anyiro cha nafasi hiyo kutoka Halmashauri Kuu kupelekwa Mkutano Mkuu ni Dk. Benson Bagonza wa Dayosisi ya Karagwe, Dk. Abednego Keshomshahara wa Dayosisi ya Kaskazini Magharibi na Dk. Blaston Gaville wa Dayosisi ya Iringa.

Nipashe ilifika mapema katika ukumbi huo na kujulishwa kuwa kikao kitaanza muda wowote baada ya kukamilika kwa ibada iliyokuwa ikiendelea ukumbini.

"Tukimaliza ibada, Halmashauri Kuu ya Kanisa itaanza utaratibu wa kupokea majina matatu ya maaskofu yaliyopata kura nyingi na hao ndio watakuwa wagombea wetu na mchakato unakwenda vizuri kuliko hayo yanayosemwa mitandaoni," kilisema chanzo chetu, mmoja wa maofisa wanaoshughulika na uratibu wa mkutano huo.

**MCHAKATO UCHAGUZI**

Kwa mujibu wa Katiba ya KKKT, katika hatua ya kwanza Mkuu wa Kanisa ataitisha faragha ya maaskofu walioko kazini kwa makusudi ya kuimarishana, kuzungumza na kuombea agenda ya uchaguzi na itaitishwa kabla ya Halmashauri Kuu.

Halmashauri Kuu katika kikao kitakachotangulia mkutano mkuu, itapendekeza majina yasiyozidi matatu na kuyapeleka mbele ya mkutano mkuu ili yapigiwe kura na mchakato wa kupata majina hayo matatu umeainishwa kikatiba.

Kila mjumbe wa Halmashauri Kuu ataandika majina matatu kutoka miongoni mwa maaskofu wanaoongoza Dayosisi za KKKT, majina yatakayoongoza ndiyo yatakayopendekezwa mbele ya mkutano mkuu wa uchaguzi mkuu wa Kanisa.

Mkutano mkuu utayapokea majina matatu kutoka Halmashauri kuu na unayo haki ya kuongeza jina moja ikibidi na utaratibu wa kupiga kura utakuwa wa kura ya kuandika na ya siri.

Mwenyekiti wa uchaguzi wa Mkuu wa Kanisa, atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Kanisa miongoni mwa wajumbe na Mkutano Mkuu utawachagua watu watano kwa ajili ya kuhesabu kura.

Wakati wa kupiga kura, kila mjumbe mwenye haki ya kupiga kura, atachagua jina moja kutoka katika majina yaliyowasilishwa mbele ya mkutano mkuu na mshindi lazima apate kura zisizopungua theluthi mbili ya kura zilizopigwa.

Kama mshindi hatapatikana katika duru ya kwanza, majina mawili yenye kura nyingi yataingia duru ya pili na iwapo kura ya theluthi mbili haitapatikana baada ya kupiga kura, uchaguzi utaingia duru ya tatu ambayo mshindi atatangazwa kwa wingi wa kura.

**WAKUU TANGU 1963**

Tangu kuanzishwa kwa KKKT mwaka 1963, wakuu walioliongoza kanisa hilo, dayosisi na miaka kwenye mabano ni Askofu Dk. Stephano Moshi (Kaskazini - 1963 hadi 1976) na Askofu Dk. Sebastian Kolowa (Kaskazini Mashariki - 1976 hadi 1992).

Wengine ni Askofu Dk. Samson Mushemba (Kaskazini Magharibi - 1992 mpaka 2007), Askofu Dk. Alex Malasusa (Mashariki na Pwani (2007 hadi 2016) na Askofu Dk. Shoo kutoka Dayosisi ya (2016 mpaka sasa).

**•Imeandikwa na Godfrey Mushi na Allan Isaack**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA
Tarehe: 24/08/2023

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **Jumanne tarehe 28-08-2023** kampuni ya **HAINAN INTERNATIONAL LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **SINGIDA** kuelekea **DAR ES SALAAM**, Gari hilo lenye namba za usajili: **T 175 DFN/T 168 DFN**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **18:00** |
| **Upana** | - | **mita** | **2.80** |
| **Kimo** | - | **mita** | **5.00** |

3. Njia itakayotumika **DAR ES SALAAM hadi IRINGA kupitia MOROGORO ROAD.** Gari itasafiri muda wa mchana tu ***( kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka 12:00 jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakao jitokeza.***

## TTCL yaanika mikakati kujenga uchumi kidijitali

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA la Mawasiliano Tanzania (TTCL) limetaja mikakati yake ya kujenga Tanzania kwenda uchumi wa kidigitali na kuongeza kasi ya kutoa huduma ya mawasiliano ndani na mipaka ya Tanzania.

Pia, limesema katika kuwezesha watu kupata huduma za intaneti kwa kasi kubwa, ifikapo Januari mwakani, wilaya 100 kati ya 139 zilizopo zitakuwa zimefikiwa na hadi Desemba, mwakani, wilaya zote nchini zitakuwa zimefikiwa.

Mkurugenzi Mkuu wa TTCL, Mhandisi Peter Ulanga, aliyasema hayo jana Dar es Salaam wakati wa mkutano na wahariri wa vyombo vya habari chini ya Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF).

"TTCL ni kitovu cha kwanza cha kuwezesha uchumi wa kidigitali nchini. Inaendesha mkongo wa taifa wa mawasiliano na kutoa huduma ijulikanayo kama 'Faiba Mlangoni Mwako' ambayo inalenga kufikisha huduma za mawasiliano ya intaneti katika makazi ya watu. Lengo letu ifikapo mwaka 2027 nyumba milioni moja ziwe zinatumia 'fiber'.

"Tunahakikisha wananchi wanaotumia huduma za mtandao za gharama nafuu na kufikika sehemu mbalimbali. TTCL imejipanga kuzifikia wilaya zote 139. Tulikuwa tunakumbana na changamoto kwenye baadhi ya wilaya kama Mafia ambayo iko baharini lakini tumeshapata suluhisho nako tutafika kipindi kijacho cha miezi minne au mitano," aliongeza.

Ulanga alisema watu wanapoona maendeleo makubwa ya mawasiliano, wafahamu kuwa TTCL ndiyo mhimili mkuu wa uendelevu wa uchumi kidigitali.

Alisema wanapozungumzia uchumi wa kidigitali, mambo mengi yatapita kwenye mitandao na TTCL ikiwa ni sekta wezeshi inayofanya kazi kwa karibu na sekta ya fedha kuhakikisha wanaboresha matumizi hayo huduma kimtandao.

"Tuko katika mazungumzo chini ya usimamizi wa wizara yetu kuhakikisha tuachane kabisa na matumizi ya fedha. Tunaweka miundombinu wezeshi maeneo mbalimbali, kipingamizi kilikuwa kutopatikana kwa miundombinu ya mawasiliano ya uhakika. Tunahakikisha kuwapo kwa mawasiliano ya uhakika ili kuingia katika huduma za kimtandao zaidi," alisema.

Alitaja faida tatu kiuchumi kuwa ni kuweka kumbukumbu sahihi za fedha maeneo mbalimbali, kurahisisha uwezo wa kukopa na kupeleka miamala sehemu mbalimbali na kuweka huduma za kifedha kuwa rahisi kwa watumiaji. "Sekta ya mawasiliano ina pambana na changamoto mbalimbali, mojawapo ikiwa miundombinu haikuwa wezeshi ndiyo maana kazi kubwa inafanyika kuongeza upatikanaji wake. TTCL tumelibeba na tunawawezesha wenzetu kampuni zote za binafsi zitumie miundombinu hiyo.

HABARI KITAIFA

# Waagizaji mafuta wakwama kisa Dola

**Na Beatrice Shayo**

CHAMA cha Waagizaji Mafuta Tanzania (TAOMAC) kimesema wanachama wake bado wanashindwa kupata mafuta kutokana na kukosekana kwa Dola ya Kimarekani ili wafanye malipo hatua ambayo pia imewafanya waendelee kupata hasara.

Mkurugenzi Mtendaji wa TAOMAC, Raphael Mgaya, katika mahojiano kwa njia ya simu na Nipashe jana, alisema bado wameshindwa kuyatoa mafuta yaliyoko katika matangi kutokana na tatizo hilo la dola tangu Machi mwaka huu, na kwamba hali imekuwa mbaya.

Alisema wao ni waauzaji wa jumla wa mafuta na kutokana na tatizo hilo, wamejikuta wanapata hasara na kulazimika kuchukua mikopo benki ya gharama kubwa. "Pia tumeshindwa kupokea mafuta kwa wakati. Mafuta yamebaki kwenye matangi huku tukilazimika kulipa gharama za kuhifadhi mzigo kwenye matangi. Tangu mwaka jana hili tatizo la dola lilianza lakini kuanzia Machi, mwaka huu, hali imekuwa mbaya zaidi.

"Sisi tunauza mafuta jumla yaani mafuta yetu yanakuja na kukaa kwenye matangi kwa ajili ya kuwauzia wafanyabiashara wa rejareja. Mafuta tunayo lakini changamoto ni kwamba tumeyanunua ila hatuwezi kuyapata kwa sababu hatuna dola, hivyo yamebaki kwenye mikono ya mzabuni," alisema.

Mgaya alisema mzabuni lazima alipwe dola zake ndipo akabidhi mafuta na kama hajalipwa yanakuwa chini ya kifungo cha kifedha, yaani ni mzigo ambao unaingia kwenye tangi umiliki unabaki kwa mzabuni na hayawezi kutoka na zaidi ya asilimia 90 ni kampuni za nje ya nchi.

"Mafuta yanaweza kuwapo lakini hatuwezi kuyauza yote kwa sababu kuna yale ambayo bado hatujamilikishwa kwa sababu ya kutokuwa na Dola za kuyalipia" alisema.

Aidha, Mgaya alisema wanachama wenzake kila siku wanalalamika wameshindwa kupata dola ya kutoa mafuta na kama dola zipo iweje hawazipati.

"Hili tatizo si la kampuni moja. Ni kampuni nyingi zimekosa Dola bado, kwa kuwa upatikanaji wa Dola una changamoto na yapo mafuta ambayo kampuni imeshindwa kuyachukua kwa sababu ya kukosa Dola ya kuyalipia kwa wakati,"alisema.

Agosti 22, mwaka huu, Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ilisema ina akiba ya kutosha ya fedha za kigeni zinazoweza kutosheleza kwa miezi mitano na kueleza mikakati ya kukabiliana na upungufu wa fedha hizo nchini.

Kiwango cha fedha za kigeni kilichopo nchini kwa upande wa Dola ya Marekani ni asilimia 77, Yuan ya China asilimia 16, Pauni ya Uingereza asilimia 4.78 na dola ya Australia 1.72.

Mkurugenzi wa Utafiti na Sera wa BoT, Suleiman Misango, alisema hayo wakati akizungumza na wahariri na waandishi wa habari Dar es Salaam, akieleza mwenendo wa hali ya fedha za kigeni nchini na hali iliyochangia upungufu wa Dola za Kimarekani.

Alitaja mikakati iliyochukuliwa kukabiliana na tatizo hilo kuwa ni BoT kuendelea kutumia akiba hiyo kuongeza ukwasi katika soko la fedha za kigeni nchini.

Misango alisema kuanzia Agosti 21, mwaka huu, BoT imeuza katika soko la fedha za kigeni Dola milioni 100.5 ikilinganishwa na Dola milioni 62 katika kipindi cha Julai - Septemba, mwaka jana.



Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, Jaji Francis Mutungi akizungumza na viongozi wa Chadema, Mwenyekiti Freeman Mbowe na Katibu Mkuu, John Mnyika ofisini kwake jijini Dar es Salaam jana kwa lengo la kuimarisha demokrasia ya vyama vya siasa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Mikoa 10 yahadharishwa El-Nino

**Na Faustine Feliciane**

WAKULIMA katika mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Mara, Kagera, Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Tanga pamoja na halmashauri katika jiji la Dar es Salaam wametakiwa kuchukua tahadhari kutokana na mvua ya El-Nino inayotarajiwa kuanza kunyesha mwishoni mwa mwezi ujao.

Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini (TMA) jana, ilitoa utabiri wa msimu wa mvua ya vuli kuwapo uwezekano wa asilimia 99 wa kutokea kwa El-Nino katika mikoa 10 nchini.

Mikoa mingine iliyotahadharishwa ni Pwani na baadhi ya maeneo ya mkoa wa Morogoro.

Akizungumzia utabiri huo, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dk. Ladislaus Chang'a, alisema mifumo ya hali ya hewa imeonyesha mvua hiyo itanyesha kwa kiwango cha juu ya wastani hadi wastani katika mikoa tofauti inayopata mvua ya vuli.

"Tumetoa angalizo na tahadhari kwa sekta mbalimbali kama kilimo pamoja na mamlaka za jiji kutokana na mvua hii, tunatarajia italeta athari chanya na hasi kwa baadhi ya maeneo, ni vyema kujiandaa na kukabiliana na athari zake," alisema Dk. Chang'a.

Alisema katika mikoa ya Kanda ya Ziwa, kunatarajiwa kuwa na mvua kubwa itakayonyesha mpaka mwanzoni mwa mwezi Januari mwakani sawa na mikoa ya Dar es Salaam, Zanzibar, Pwani na baadhi ya maeneo ya mkoa wa Morogoro.

"Mvua hii huenda ikaleta athari kwenye miundombinu katika Jiji la Dar es Salaam, lakini pia itaathiri ukuaji wa mazao katika mikoa tajwa," alisema Dk. Chang'a. Alisema katika maeneo mengi mvua hiyo inatarajiwa kuanza kunyesha mwishoni mwa mwezi ujao na kumalizika mwishoni mwa mwezi Desemba na mikoa mingine itamalizika Januari, mwakani.

"Lakini mvua hii italeta faida kwa sekta ya mifugo, tunatarajia unyevunyevu katika maeneo mengi kutastawisha majani hivyo malisho ya wanyama yatakuwa ya uhakika," alisema Dk. Chang'a.

Pia, sekta ya afya imetahadharishwa kuchukua hatua kukabiliana na magonjwa ya mlipuko yanayoweza kutokea kutokana na mvua hiyo. Alisema, wananchi na wadau wanashauriwa waendelee kufuatilia taarifa za hali ya hewa zitakazotolewa na mamlaka hiyo kupitia vyombo vya habari.

## Watumishi TANESCO wasomewa mashtaka 125

**Na Remmy Moka,** SAUT

WATUMISHI wawili wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) Wilaya ya Nyamagana, mkoani Mwanza, wamepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mwanza wakikabiliwa na mashtaka 125 ya uhujumu uchumi ikiwa ni pamoja na kuisababishia serikali hasara ya Sh. bilioni mbili.

Washtakiwa hao ambao ni fundi mchundo Abdulkadir Lwassa (39) na Ofisa Bohari, Respicius Rwegoshora (33), walifikishwa mahakamani huko juzi, wakikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi namba 5/2023.

Walisomewa mashtaka 125 yakiwamo ya kughushi nyaraka za serikali, ubadhirifu wa mali za umma na kutoa nyaraka za uongo.

Akisoma mashtaka hayo mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Stella Kiama, Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Maximilian Kyabona, alidai washtakiwa hao walitenda makosa hayo kati ya Novemba 16, 2021 na Desemba 17, 2022 katika ofisi za bohari ya TANESCO iliyoko Nyakato, Mwanza.

Kyabona aliiomba mahakama hiyo kuahirisha kesi hiyo kwa kuwa upelelezi haujakamilika.

Kyabona alidai kuwa upelelezi wa shauri hilo unaendelea na kuiomba mahakama kupanga tarehe ya kutajwa kwa kesi hiyo.

Washtakiwa wanatetewa na mawakili watatu; Amri Linus, Erick Mutta na Steven Kitale ambao waliomba upande wa Jamhuri kukamilisha upelelezi haraka kama ilivyoelekezwa na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali.

Hakimu Kiama baada ya kusikiliza pande zote mbili, alisema kutokana na hoja hizo, washtakiwa wataendelea kubaki mahabusu hadi Septemba 4, 2023, kesi itakapotajwa.



Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), Victor Seff, akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dodoma kuhusu utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya wakala huo na mwelekeo wa mwaka wa fedha 2023/24. **PICHA PAUL MABEJA**

# CMSA yabariki CRDB kutoa hatifungani ya kijani

## -Ni kubwa zaidi kusini mwa Jangwa la Sahara; itauzwa DSE na LSE kuwezesha miradi ya mazingira

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuongeza uwezo wake wa kufanya uwezeshaji wa miradi rafiki kwa mazingira, Benki ya CRDB imepata idhini kutoka Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) kuuza Hatifungani ya Kijani (Green Bond) yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 300 (Sh. bilioni 780).

Hatua hiyo inafanya CRDB kuweka historia ya kuwa taasisi ya kwanza kutoa hatifungani ya kijani nchini inayoweka mkazo katika masuala ya mazingira na kubwa zaidi kusini mwa Jangwa la Sahara.

Wakati wa kupokea idhini ya kuuzwa kwa hatifungani hiyo jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema ni furaha kubwa kwao kupata idhini kutoka CMSA kuuza hatifungani hiyo ambayo lengo lake si tu kupata rasilimali fedha, bali pia kufanikisha utekelezaji wa miradi yenye mrengo wa kuhifadhi mazingira, hivyo kushiriki ipasavyo katika mapambano dhidi ya mabadiliko ya tabianchi.

"Pamoja na kuwa Benki ya CRDB inaweka rekodi ya kuwa taasisi kubwa zaidi ya fedha nchini kupata idhini ya kuuza hatifungani ya kijani, benki yetu sio ngeni katika uwezeshaji wa miradi yenye mrengo wa utunzaji wa mazingira kwa kuwa Novemba 2019 ilitambuliwa na kuingia makubaliano na Mfuko wa Mazingira wa Umoja wa Mataifa (GCF) kufanikisha miradi ya kulinda mazingira.

"Hii pia ilikuwa ni mara ya kwanza benki ya biashara kusini mwa Jangwa la Sahara kutunukiwa sifa hiyo na tangu hapo, tumeshiriki kwa kiasi kikubwa kuwezesha miradi inayokusudia kulinda mazingira," alisema Nsekela.

Kuhusu uwezeshaji wa miradi ya mazingira, Nsekela alisema kwa mwaka jana pekee, Benki ya CRDB ilikopesha jumla ya Sh. trilioni 6.978 ambazo ni sawa na asilimia 26 ya mikopo yote iliyotolewa na taasisi za fedha nchini.

Kati ya fedha hizo, Nsekela alisema Sh. bilioni 1.44 zilikopeshwa katika sekta ya misitu, kiwango ambacho ni sawa na asilimia 55 ya mikopo yote iliyotolewa kwenye sekta ya misitu. Kwenye kilimo, sekta muhimu kwenye uhifadhi wa mazingira na inayotoa ajira nyingi zaidi nchini na kulipa Taifa fedha nyingi za kigeni, alisema Nsekela benki hiyo ilikopesha Sh. trilioni moja ambazo ni sawa na asilimia 43 ya mikopo yote iliyotolewa katika eneo hilo na ikapeleka Sh. bilioni 55.88 katika sekta ya nishati mbadala.

Licha ya jitihada hizo, mkurugenzi huyo alisisitiza kuwa bado kuna mahitaji makubwa ya fedha kuliko uwezo walionao, hivyo kutafuta namna rafiki ya kufanikisha suala hilo.

"Kwa kutambua mahitaji yaliyopo, Benki ya CRDB imeona ni muhimu kutafuta vyanzo vipya vya fedha kuwezesha miradi hii. Leo (jana) nina furaha kuona jitihada zetu zimezaa matunda kwa CMSA kutupa idhini ya kuuza hatifungani yetu ya kijani (green bond) ambayo itauzwa kwa awamu tano. Katika awamu hii ya kwanza tunatarajia kupata Sh. bilioni 55," alisema Nsekela.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa CMSA, Nicodemus Mkama, ameipongeza Benki ya CRDB kwa kufanikiwa kuwa benki ya kwanza nchini kupata idhini ya kutoa hatifungani itakayowezesha kupata fedha za kutekeleza miradi ya kuhifadhi mazingira na matokeo chanya kwa jamii (green, social and sustainability bond).

Alisema idhini imetolewa na CMSA baada ya Benki ya CRDB kukidhi matakwa ya Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana Sura ya 79 ya Sheria za Tanzania; Miongozo ya Utoaji wa Hatifungani, kuwapo muundo wa hatifungani; Kanuni za Jumuiya ya Kimataifa ya Masoko ya Mitaji (ICMA); na kupata ithibati kutoka kwa taasisi zenye utaalam kuhusu miradi ya kuhifadhi mazingira na matokeo chanya kwa jamii.

Alisema Benki ya CRDB imekidhi matakwa hayo na kupata ithibati kutoka Taasisi ya Uendelezaji wa Sekta za Fedha Barani Afrika (FSD Africa) na Taasisi ya Sustainalytics ya Uingereza.

"Hatifungani hii inaweka historia ya kuwa hatifungani ya kwanza yenye lengo la kuhifadhi mazingira na matokeo chanya kwa Jamii kutolewa nchini na katika ukanda wa kusini mwa Jangwa la Sahara.

Mkama alifafanua kuwa utoaji wa hatifungani hiyo ni hatua muhimu katika ustawi na maendeleo ya sekta ya fedha na uchumi nchini, kwa kuwa utachangia katika utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha wa 2020/21-2029/30 wenye lengo la kuwezesha upatikanaji rasilimali fedha kwa ajili ya miradi katika sekta ya umma na binasi ili kujenga uchumi shindani kwa maendeleo ya watu.

Mkama alisema CMSA imeidhinisha utoaji wa hatifungani hiyo itakayotoa mikopo kwa Shilingi na fedha za kigeni (multicurrencies) kutokana na mazingira wezeshi na shirikishi ya kisera, kisheria na kiutendaji ya serikali.

Mkama alitoa rai kwa wadau wote wa sekta ya fedha kuendelea kushirikiana na serikali kupitia CMSA katika kutekeleza mikakati ya upatikanaji fedha za kutekeleza miradi na shughuli za maendeleo kwa kutoa bidhaa mpya na bunifu zenye lengo la kuhifadhi mazingira, na zenye mguso na matokeo chanya kwa jamii, hivyo kuchangia katika kuchochea maendeleo ya jamii na ukuaji wa uchumi nchini.

Akiishukuru CMSA na wadau wengine walioshiriki mchakato mzima mpaka kupatikana kibali hicho, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya CRDB, Dk. Ally Laay, alisema wawekezaji wa ndani na watokao nje wanayo fursa ya kunufaika na hatifungani hiyo kwa kuwa mikopo itapatikana kwa Shilingi au dola ya Marekani. "Mara nyingi, Benki ya CRDB imekuwa ya kwanza. Leo hii ni fursa nyingine kwa benki hii kuorodhesha hatifungani kubwa zaidi, sio nchini pekee bali kwa nchi zote za kusini mwa Jangwa la Sahara. Ninawashukuru CMSA na Soko la Hisa Dar es Salaam (DSE) na wadau wengine waliotusaidia kufanikisha hili. Ninawaomba Watanzania wenzangu kujitokeza kununua hatifungani hii pindi itakapoanza kuuzwa muda si mrefu kutoka leo. Tusiiache fursa hii itupite," alisema Dk. Laay.

## Mchakato wa mbunge kufikishwa kortini waiva

**Na Waandishi Wetu,** ARUSHA

MCHAKATO wa kumburuza mahakamani Mbunge wa Ngorongoro (CCM), Emmanuel Ole Shangai na wananchi wengine wanaotuhumiwa kuhusika katika tukio la kuvamia na kushambulia waandishi wa habari, Agosti 15 mwaka huu katika Kata ya Enduleni, wilayani Ngorongoro umeiva.

Jalada lenye mashtaka yanayomkabili mbunge huyo na wenzake limepelekwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (NPS) kwa hatua zaidi za kisheria.

Ole Shangai na wenzake ambao idadi yao haijawekwa wazi na Jeshi la Polisi, walishikiliwa kwa siku kadhaa, wakihojiwa kuhusiana na tukio la vijana wa rika wa jamii ya kifugaji ya Kimasai wanaokadiriwa kuwa zaidi ya 300, kuwavamia na kuwajeruhi waandishi wa habari mbalimbali waliokuwa wakitekeleza majukumu yao.

Jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Kamishna Msaidizi Justine Masejo, alithibitisha upelelezi wa tukio hilo umekamilika na jalada limepelekwa NPS.

Wakati Kamanda Masejo akieleza kukamilika kwa upelelezi wa tukio hilo, Mbunge Ole Shangai aliachiwa kwa dhamana juzi saa 3:00 usiku, alipokuwa ameshikiliwa katika Kituo cha Polisi cha Diplomasia kilichoko Karatu.

"Nimetoka (nimeachiwa) kwa kupewa dhamana. nilikamatwa Agosti 21 mwaka huu, nilipokuja mwenyewe kuripoti. Nilikuwa kituoni Karatu kwa siku tatu, sikula chakula na nipo vizuri kwa sababu walinipa chakula sikutaka kula kwa kuwa huwezi kula chakula cha mtesi wako. Nimejifunza tu kuwa ninaweza kutokula kwa siku tatu na nikawa vizuri tu," alisema Ole Shangai

Kwa mujibu wa Ole Shangai, baada ya kutakiwa kuripoti polisi, alikwenda Kituo cha Polisi Melela, ambako alifuatwa na ofisa aitwaye afande Felo na kujitambulisha kwake kuwa ni Msaidizi wa Mkuu wa Upelelezi wa Wilaya ya Karatu, wakamhoji kwa zaidi ya saa tano kisha wakamtoa kumpeleka Karatu Kituo cha Diplomasia, majira ya saa 7:32 usiku na kufika Karatu saa nane usiku.

Aliwasihi wananchi kutokuwa na wasiwasi kwa kuwa yuko pamoja nao na ataendelea kupaza sauti zao na hatoacha kwa kuwa anafahamu "hizo ni siasa tu" na atatakiwa kuripoti polisi Jumatatu ya wiki ijayo.

Alipotafutwa kuzungumzia jambo hilo, Wakili Joseph Ole Shangai anayewawakilisha wananchi 31 wanaodaiwa kushikiliwa, alisema:

"Walikamatwa watu Agosti 16, mwaka huu, hadi leo (juzi) hawajafikishwa mahakamani kwa tuhuma za kujeruhi na pia wanahojiwa kuhusu kuhamia Msomera."

Wakili Alais Melau, alisema kati ya hao wanaoshikiliwa, mmoja ni mgonjwa wa kifua kikuu na alikamatwa akiwa anatoka kuchukua dawa.

**•Imeandikwa na Cynthia Mwilolezi na Godfrey Mushi**

# Mahakama yatengua hukumu kifungo cha maisha

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Rufani Moshi imemwachia huru kwa kumwondolea hati na adhabu ya kifungo cha maisha jela, raia wa Liberia, Grace Gbatu, baada ya kuona ushahidi wa upande wa mashtaka ulikuwa na makosa ya kisheria.

Hukumu hiyo ya mahakama ilitolewa juzi na jopo la majaji watatu, Jaji Jacob Mwambegele, Abrahman Mwampashi na Benhajj Masoud baada ya kusikiliza ushahidi wa pande zote mbili.

Grace alifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi, akikabiliwa na kosa la kusafirisha dawa za kulevya. Inadaiwa kuwa Desemba Mosi 2013, katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), wilayani Hai, mkoani Kilimanjaro, mrufani alikutwa akisafirisha gramu 10.064 za heroin.

Mrufani alikana mashtaka, lakini baada ya usikilizwaji wa shauri kumalizika, alitiwa hatiani na kuhukumiwa kwenda jela kutumikia kifungo cha maisha. Mrufani hakukubaliana na hukumu, akakata rufani.

Inadaiwa kuwa ushahidi uliotolewa mahakamani, mrufani alikamatwa maeneo ya KIA, akielekea Free Town kupitia Nairobi,Kenya. Alikuwa na mabegi mawili ambayo baada ya kuwekwa kwenye mashine ya ukaguzi, yalibainika kuna vitu vyenye shaka ambavyo picha zake hazikuonekana vizuri.

Inadaiwa mabegi hayo mawili yenye jina la mrufani, yalichukuliwa na maofisa usalama waliokuwa zamu. Alipoulizwa kuhusu mabegi hayo alikiri ni mali yake. Mrufani aliagizwa kufungua mabegi hayo, yalionekana kabeba nguo na vitu binafsi. Vitu vyote vilitolewa, lakini mabegi yalionekana bado mazito.

Mabegi yalirejeshwa katika mashine ya ukaguzi, lakini vitu visivyo vya kawaida vilionekana tena. Mabegi hayo yalichanwa na ndani yake ilikutwa mito ya sponji iliyokuwa imejazwa unga uliodhaniwa kuwa dawa za kulevya.

Tukio liliripotiwa kwa Mkuu wa Usalama aliyekuwa zamu, alikwenda eneo la tukio na maafisa wawili. Walipofika walikuta begi lingine likifunguliwa na mito mingine minne ilikutwa na unga uliodhaniwa kuwa ni dawa za kulevya.

Baada ya hapo, mrufani alifikishwa Kituo cha Polisi cha KIA, unga ulikwenda kufanyiwa uchunguzi kwa Mkemia Mkuu wa Serikali na kubainika ulikuwa dawa za kulevya.

Inadaiwa katika utetezi wake, mrufani alikataa kuhusika na dawa hizo za kulevya na kuiambia mahakama kwamba alifika Tanzania Novemba 22, 2013 kumtembelea mpenzi wake, Jack Benson.

Anadai siku ya tukio, alikuwa KIA, akirejea nyumbani kwao, alipofika dawati la uhamiaji mmoja wa maofisa usalama alimsogelea akataka kumpekua, alimwachia mabegi akaendelea na ukaguzi.

Anadai ofisa huyo alimwambia mabegi hayo yalikuwa na shida ndipo yalipochukuliwa na kuingizwa kwenye chumba, yakachanwa, unga ulikutwa, akashikiliwa na kupelekwa Moshi, kisha kufikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi.

Baada ya shauri lote kusikilizwa, Mahakama Kuu Moshi, ilikubali kwamba upande wa mashtaka umeweza kuthibitisha mashtaka dhidi ya mrufani pasipo kuacha shaka, mrufani akatiwa hatiani kwa kosa la kusafirisha dawa za kulevya aina ya heroin gramu 10 na kuhukumiwa kifungo cha maisha.

Aliwasilisha rufani kupinga kutiwa hatiani na adhabu akiwa na sababu 19. Kati ya sababu hizo, mahakama ilizingatia sababu moja ya saba ambayo ni jaji alikosea kisheria na mantiki kukubali au kuamini katika kielekezo cha pili ambacho ni bahasha nne za kaki zilizowekwa mito ya sponji na kilichomo ndani yake.

Mjibu maombi aliwakilishwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Cecilia Mkonongo, akisaidiana na Henry Chaula Wakili wa Serikali.

Mrufani anadai kielekezo hakikuwa katika orodha ya vielelezo vilivyotajwa wakati wa usomwaji wa maelezo ya mashahidi wala usikilizwaji wa awali.

Pamoja na upungufu huo, Wakili Cecilia aliendelea kupinga rufani hiyo, akidai haijalishi kama kiliandikwa lakini katika hati ya ukamataji iliandikwa na kielelezo hicho kilitolewa mahakamani, hivyo hoja hiyo inapaswa kupuuzwa.

"Baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili, tumebaini hakuna ubishi kwamba kielelezo namba mbili hakikuorodheshwa wala kutajwa katika maelezo ya mashahidi, wala kusomwa katika maelezo hayo na hakikusomwa pia katika maelezo ya awali.

"Kielelezo hakikutajwa kokote kama upande wa mashtaka walikitegemea katika kesi hiyo. Ni hoja ya kawaida kwamba vielelezo asilia ambavyo upande wa mashtaka wana nia ya kuviwasilisha na kuvitegemea katika kesi vinapaswa kuorodheshwa au kutajwa wakati wa kusoma maelezo ya mashahidi na kushindwa kufanya hivyo ni ukiukwaji wa sheria. "Ni wazi kuwa Wakili Mkonongwa alikubaliana na sheria kwamba ni takwa la sheria sio tu kusoma na kufafanua kwa mtuhumiwa taarifa zinazowasilishwa dhidi yake, lakini pia ni takwa la sheria kuorodhesha vielelezo asili ambavyo upande wa mashtaka wana nia ya kuviwasilisha katika ushahidi na kuvitegemea katika kesi.

"Kutokana na sababu zilizotolewa na nyinginezo, tunaikubali rufani na kumwondolea hatia pamoja na kifungo cha maisha. Mrufani atolewe gerezani isipokuwa kama ana makosa mengine," liliamuru jopo.


## NOTISI/TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,YARDLEY RECOVERIES AUCTION LTD, SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya Benki ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| KIJITONYAMA | NEZAK INVESTMENT LTD | 1.NYUMBA YENYE HATI NA. DSMT1019002 KIWANJA NAMBA P23439 KIFURU-KINYEREZI 2.NYUMBA YENYE HATI NA. 70437 KIWANJA NA. '213', KITALU '14' BUNJU KINONDONI , 3.NYUMBA YENYE HATI NA. 192019 KIWANJA NA. '130', KITALU 'N' PUGU MWAKANGA | 1. ZACHARIA ANTHONY KAPAMA 2.DAFROSA ATHONY KAPAMA 3. RASHIDI ALLY | 1.KIFURU KINYEREZI-ILALA 2.BUNJU KINONDONI 3.PUGU MWAKANGA | 28/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEGETA | LUCAS NTIRUHUNGWA MZYENGE | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | JAPHET YONA MZAVA | KIGAMBONI | 12/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | BAHATI YOHANA NYATO | MOTOR VEHICLE SCANIA TRACTOR T163 DCV | BAHATI YOHANA NYATO | MAKAMBAKO | 08/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBAGALA | MAMU PHARMACY | 1.NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA.151,KITALU 'Q10' HATI NAMBA 143195-KIBAMBA 2.NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO-CHAMAZI DOVYA | AHMAD KASSIM OMARY | 1.KIBAMBA 2.CHAMAZI DOVYA | 31/08/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KIJITONYAMA | MUSTAFAH IDD GEKE | NYUMBA | MUSTAFAH IDD GEKE | MABWEPANDE | 14/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | SELEMANI CHARLES MNIKO | NYUMBA | SELEMANI CHARLES MNIKO | MBUGANI -MWANZA | 8/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | T/A NINIGANI DEPOT EDWARD | NYUMBA | EDWARD JEREMIA MASSASI | MIHAMA BWIRU | 31/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | EMMANUEL LUKINDA LUTIMA | BUS TATA T847 DKN | EMMANUEL LUKINDA LUTIMA | MWANZA MJINI | 30/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | FRIDA FRANCIS KAJUNA | NYUMBA | FRIDA FRANCIS KAJUNA | GEITA | 30/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | NOZAWA G DAVID,MR. T/A BUSWELU SATELITE CABLE NETWORK | KIWANJA | KATONGOLE DASTAN | NORTH BUSWELU-MWANZA | 05/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | JOSEPH MAKALA MAKALA | NYUMBA | JOSEPH MAKALA MAKALA | NYASAKA ILEMELA MWANZA | 29/08/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | JAMES JACOB KALULEMA | NYUMBA | JAMES JACOB KALULEMA | MAHINA KANYERERE-MWANZA | 29/08/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.

2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.

3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.**0745707008/0787129539/0714939933/0655715138**

4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

217570302

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# 'Tusitegemee kilimo pekee, tuangalie mifugo, uvuvi'

**WATANZANIA** wametakiwa kubadili mtazamo kutoka kutegemea mazao ya kilimo pekee bali kujumuisha mifugo na uvuvi katika uhakika wa chakula na maendeleo kwa ujumla.

Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika litawakutanisha wakuu wa nchi, mawaziri, mabalozi, wakulima, wafugaji, wavuvi na wadau wengine kutoka nchi zote za Afrika zaidi ya 3,000, kujadili mambo muhimu ya kuendeleza sekta hizo.

Kwa mara ya kwanza wadau wa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi wanashirikiana kukamilisha mkutano huo kutokana na sekta hizo kutegemeana na lazima kuwa na ujumuishi.

Mkutano huo ni muhimu ni kielelezo cha mafanikio ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan na kupitia jukwaa hilo watajifunza teknolojia mpya zitakazosaidia kukuza kilimo, mifugo na uvuvi ikiwamo kuyafikia masoko.

Ikizingatiwa kuwa mazao ya mifugo na uvuvi yana protini nyingi ambayo inasaidia afya ya mwili, lakini na kuchagiza maeneo ya ufugaji kama kuku na wanyama wengine ndiyo maana Wizara ya Kilimo imeona umuhimu wa kujumuisha.

"Tunataka tunapokwenda kwenye mkutano huu tuna uelewa wa pamoja kuhusu dhumuni, malengo na nia. Mkutano huu ni fursa kwa Tanzania kulisha Afrika na dunia kwa ujumla ikiwa tutazalisha chakula kwa wingi," alisema Waziri mwenye dhamana Abdallah Ulega.

Kaulimbiu ya mkutano huo ni 'Vijana na Wanawake ndiyo kiini cha uzalishaji na mabadiliko katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi.

Wizara hiyo imeanzisha Programu ya Building a Better Tomorrow (BBT-Mifugo) ili kutengeneza wafanyabiashara wa mifugo na uvuvi na kuna mpango wa kupeleka Shilingi bilioni sita kwenye sekta hizo ili kuzalisha kisasa na kuyafikia masoko.

"Soko lipo duniani ni muhimu kwa nchi zetu kuongeza uzalishaji na kuuza nje, tutafute mitaji, teknolojia ya kisasa ili kuondoka kuzalisha kwa ajili ya chakula cha familia bali kibiashara, ndiyo maana tumekuja na BBT ili tuwe na vijana wanaochangamkia fursa hizi."


Mchumi wa Kilimo kutoka Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo (ILRI), anasema lengo ni kuhakikisha sekta zote za uzalishaji zinafikika kwa mazingira wezeshi kwa kuhakikisha pembejeo zinapatikana.

Pia ni muhimu kutambua mchango wa mifugo na uvuvi katika kukabili mabadiliko ya tabianchi na kwamba ni ukweli kuwa mtu anapokula chakula hakifurahii kama hakina nyama jambo linaloonyesha kuna kuhitajiana.

Meneja Mkazi wa Taasisi ya Kilimo Barani Afrika (AGRA), Vianey Rweyendela anakumbusha ushindani mkubwa uliokuwapo wa mahali pa kufanyia mkutano, lakini kutokana na utashi wa kisiasa wa Rais Samia ndiyo umesaidia.

Ni mara ya kwanza kwa Jukwaa hili linapokwenda kwenye nchi nyingine na kuzinduliwa na Rais, "kwetu Rais Samia alifanya hivyo ikiwamo kutangaza yeye mwenyewe na pia ni mara ya kwanza kwa mifugo na uvuvi kuwa sehemu moja, tumefanya nchi nyingi ila Tanzania inafanyika kwa utofauti mkubwa,tunatarajia mafanikio makubwa."

Bila shaka mkutano huo ni muhimu na utatumika vyema kuleta tija katika sekta ya kilimo na mifugo kwa maendeleo ya nchi.






## Muungwana Lazima Nilonge

# Ukosefu wa alama za barabarani kwa baadhi ya maeneo ni kero kwa umma

Na Khadija Kategile, TUDARCo

**UKOSEFU** wa alama na taa za barabarani katika baadhi ya maeneo ya Dar es Salaam imekuwa kero kwa wakazi wa sehemu hizo na kusababisha changamoto kubwa ya usalama, hasa watumiaji wa njia hizo kama vile madereva wa vyombo vya moto na watembea kwa miguu.

Kutokana na kukosekana kwa alama hizo madereva wamekuwa wakikabiliana na vikwazo vingi vinavyofaya kuwapo kwa usalama mdogo kwao na watu wanaoishi maeneo hayo, kwani kuna uwezekano mkubwa wa ajali kutokea.

Sinza Darajani, jijini Dar es Salaam, ni mojawapo ya eneo linalokabiliwa na changamoto za kukosekana kwa taa za barabarani, hivyo kunafanya msongamano mkubwa wa magari wakati wa asubuhi na jioni, kwani sehemu hiyo inakutanisha barabara nne, foleni inakuwa kubwa.

Pia, karibu na maeneo hayo, kumejengwa shule mbili za msingi, ambazo ni Kilimani na Uzuri. Hiyo inakuwa hatari kwa wanafunzi wanaovuka eneo hilo kwenda ng'ambo ya pili, kwani bado ni wadogo na wanahitaji mwongozo sahihi wakati wa kuvuka.

Kukosekana kwa alama hizo na taa, kumefanya wakazi wa maeneo hayo kukabiliwa na changamoto kwa baadhi ya madereva wazembe ambao hawazingatii sheria za barabarani, hivyo kuwaumiza wao na mali na zao.

Aidha, eneo hilo limekuwa likikabiliwa na foleni za mara kwa mara kwani madereva wamekosa muongozo sahihi wa nini cha kufanya wafikapo katika sehemu hiyo hivyo, kupelekea kero kwa madereva na abiria.

> **Wakazi wa eneo hilo ni vyema kuiomba serikali na mamlaka za usalama barabarani kuweza kuweka alama za pundamilia na mataa ya kuruhusu watumiaji kupita ili kuboresha utendaji wa suala hilo kushughulikiwa au kufanyika haraka iwezekanavyo.**

Wakazi wa eneo hilo ni vyema kuiomba serikali na mamlaka za usalama barabarani kuweza kuweka alama za pundamilia na mataa ya kuruhusu watumiaji kupita ili kuboresha utendaji wa suala hilo kushughulikiwa au kufanyika haraka iwezekanavyo.

Serikali inapaswa kuchukua hatua za moja kwa moja katika kuweka alama za barabarani nchini na maeneo mengine yanayohatarisha usalama kwa watumiaji wa barabara hizo ili kupunguza msongamano na ongezeko la ajali.

Pia elimu ya usalama barabarani inatakiwa kutolewa kwa wakazi wote nchini kwa nia ya kuwafahamisha juu ya umuhimu wa kuzingatia sheria za usalama wa barabarani.

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alitamka kuwa "jukumu la usalama barabarani ni la kila mmoja wetu na si la serikali pekee" na akawataka wananchi wote watoe ushirikiano kuzuia ajali za barabarani,wakazi kusaidiana kutafuta suluhisho endelevu kwa tatizo hili ili kuimarisha usalama wa barabarani.

Ni muhimu sana wananchi wote wa Tanzania kila maeneo kujua na kuzingatia sheria,ili kulinda maisha yao na watumiaji wengine wa barabarani katika matumizi ya shughuli mbalimbali za jamii.

Mara zote tuzunguke tukikumbuka kuwa, **"JUKUMU LA USALAMA NI LETU SOTE"**

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com

# Waziri Ulega ataka mtazamo mpya kwenye kilimo, mifugo

**Na Salome Kitomari**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega amesema ni muhimu kubadili mtazamo kutoka kutegemea mazao ya kilimo pekee bila kujumuisha mifugo na uvuvi kwa kuwa vinakwenda sambamba katika uhakika wa chakula na maendeleo kwa ujumla.

Alikuwa akifungua mafunzo ya siku moja kwa wahariri na waandishi juzi jijini Dar es Salaam, kuhusu kazi zinazofanywa na wizara pamoja na wadau kuhusu mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula utakaofanyika Dar es Salaam Septemba 5 hadi 8, mwaka huu.

Alisema awali mkutano huo ulitambulika kama Jukwaa la Mapinduzi ya Kijani Afrika (AGRA), na kutokana na juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan sasa utakuwa ni Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika utakaowaleta pamoja wakuu wa nchi, mawaziri, mabalozi, wakulima, wafugaji, wavuvi na wadau wengine kutoka nchi zote za Afrika zaidi ya 3,000.

Alisema kwa mara ya kwanza wadau wa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi wanashirikiana kukamilisha mkutano huo kutokana na kwamba sekta hizo zinategemeana na kwamba ni lazima kuwa na ujumuishi.

"Mkutano huu ni muhimu ni kielelezo cha mafanikio ya uongozi wa Rais Samia, kupitia jukwaa hili tutajifunza teknolojia mpya zitakazosaidia kukuza kilimo, mifugo na uvuvi ikiwamo kuyafikia masoko ya nje," alisema.

Alisema mazao ya mifugo na uvuvi yana protini nyingi ambayo inasaidia afya ya mwili, na kuchagiza maeneo ya ufugaji kama kuku na wanyama wengine ndiyo maana wizara imeona umuhimu wa kujumuisha.

"Tunataka tunapokwenda kwenye mkutano huu tuna uelewa wa pamoja kuhusu dhumuni, malengo na nia. Mkutano huu ni fursa kwa Tanzania kulisha Afrika na dunia kwa ujumla ikiwa tutazalisha chakula kwa wingi," alisema Waziri Ulega.

Alisema kaulimbiu ya mkutano huo ni 'Vijana na wanawake ndio kiini cha uzalishji na mabadiliko katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi'.

Uledi alisema wizara hiyo imeanzisha Programu ya Building a Better Tomorrow (BBT-Mifugo), ili kutengeneza wafanyabishara wa mifugo na uvuvi na kwamba kuna mpango wa kupeleka Shilingi bilioni sita kwenye sekta hizo ili kuzalisha kisasa na kuyafikia masoko.

"Soko lipo duniani ni muhimu kwa nchi zetu kuongeza uzalishaji na kuuza nje, tutafute mitaji, teknolojia ya kisasa ili kuondokana na kuzalisha kwa ajili ya chakula cha familia bali kibiashara, ndiyo maana tumekuja na BBT ili tuwe na vijana wanaochangamkia fursa hizi," alisema.

Mchumi wa Kilimo kutoka Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo (ILRI), James Rao, alisema lengo ni kuhakikisha sekta zote za uzalishaji zinafikika kwa mazingira wezeshi kwa kuhakikisha pembejeo zinapatikana.

Alisema pia ni muhimu kutambua mchango wa mifugo na uvuvi katika kukabili mabadiliko ya tabianchi na kwamba ni kweli kuwa mtu anapokula chakula hakifurahii kama hakina nyama jambo linaloonyesha kuna kuhitajiana.

Meneja Mkazi wa Taasisi ya Kilimo Barani Afrika (AGRA), Vianey Rweyendela alisema kulikuwa na ushindani mkubwa wa mahali pa kufanyia mkutano lakini kutokana na utashi wa kisiasa wa Rais Samia ndio umesaidia.

"Ni mara ya kwanza kwa Jukwaa hili linapokwenda kwenye nchi nyingine na kuzinduliwa na Rais, kwetu Rais Samia alifanya hivyo ikiwamo kutangaza yeye mwenyewe na pia ni mara ya kwanza kwa mifugo na uvuvi kuwa sehemu, tumefanya nchi nyingi ila Tanzania inafanyika kwa utofauti mkubwa,tunatarajia mafanikio makubwa," alibainisha.

## Chuo Uhasibu kutoa ufadhili kozi mpya tano

**Na Beatrice Shayo**

CHUO cha Uhasibu Arusha (IAA) kimetangaza kutoa ufadhili wa masomo katika kozi mpya tano ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan katika kuongeza wataalamu nchini.

Kozi hizo zilizopo katika ngazi ya Shahada ya kwanza ni fani za fedha, ukaguzi wa hesabu, usimamizi wa mikopo, media anuwai na mawasiliano kwa umma, ukutubi na usimamizi wa nyaraka.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Eliamani Sedoyeka, akizungumza na waandishi wa habari kuwa lengo la ufadhili huo ni kuondoa vikwazo vya kifedha kwa wanafunzi na kutoa fursa sawa kwa kila atakayekidhi vigezo kusoma kozi hizo.

"Rais Samia kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia mwaka huu ametoa udhamini wa masomo kwa wanafunzi wa masomo ya sayansi maarufu kama "Samia Scholarship". Sisi kama taasisi ya elimu ya juu tumeamua kuunga mkono juhudi hizo tunatoa elimu bure kwa kozi hizo watakaopata," alisema.

Alisema chuo hicho kinatambua changamoto zinazowakabili vijana wengi katika kufikia elimu bora ikiwamo vya kifedha na kuua ndoto zao za kufikia malengo ya kielimu na kuanzisha programu hiyo ya udhamini wa masomo.

Sedoyeka, alisema udhamini huo utawalenga wahitimu wa kidato cha sita kwa mwaka 2022 na 2023 wenye ndoto na malengo ya kusoma kozi hizo wanaokabiliwa na changamoto za kifedha.

"Ili muombaji akidhi vigezo vya kupata udhamini huu ni lazima awe ameomba kujiunga na chuo chetu na kufanya udahili. Napenda kuwakaribisha wahitimu wote wenye sifa kujiunga na chuo chetu kwa ngazi ya shahada ya kwanza katika maeneo tajwa," alisema.

Alisema kupitia ufadhili huo wanatarajia kuona mafanikio makubwa kwa wanafunzi hao katika kufikia malengo yao ya kielimu na kuchangia katika maendeleo ya jamii na taifa kwa jumla.


TAARIFA KWA UMMA

airtel money

TUMA NA KUTOA PESA BILA TOZO

ADA ZA MIAMALA YA AIRTEL MONEY

TOA PESA KWA WAKALA/ATM

| Kutoka (TSH) | Kwenda (TSH) | Ada ya Airtel Money | Tozo ya Serikali | Jumla makato | Okoa Tozo | Unalipa Bila Tozo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 100 | 999 | 190 | 10 | 200 | 10 | 190 |
| 1,000 | 1,999 | 310 | 10 | 320 | 10 | 310 |
| 2,000 | 2,999 | 390 | 10 | 400 | 10 | 390 |
| 3,000 | 3,999 | 584 | 14 | 598 | 14 | 584 |
| 4,000 | 4,999 | 637 | 27 | 664 | 27 | 637 |
| 5,000 | 6,999 | 954 | 54 | 1,008 | 54 | 954 |
| 7,000 | 9,999 | 1,006 | 56 | 1,062 | 56 | 1,006 |
| 10,000 | 14,999 | 1,472 | 102 | 1,574 | 102 | 1,472 |
| 15,000 | 19,999 | 1,565 | 195 | 1,760 | 195 | 1,565 |
| 20,000 | 29,999 | 2,056 | 306 | 2,362 | 306 | 2,056 |
| 30,000 | 39,999 | 1,750 | 351 | 2,101 | | |
| 40,000 | 49,999 | 2,250 | 419 | 2,669 | | |
| 50,000 | 99,999 | 2,600 | 573 | 3,173 | | |
| 100,000 | 199,999 | 3,500 | 707 | 4,207 | | |
| 200,000 | 299,999 | 5,100 | 821 | 5,921 | | |
| 300,000 | 399,999 | 6,200 | 838 | 7,038 | | |
| 400,000 | 499,999 | 6,700 | 982 | 7,682 | | |
| 500,000 | 599,999 | 7,200 | 1,245 | 8,445 | | |
| 600,000 | 699,999 | 7,600 | 1,532 | 9,132 | | |
| 700,000 | 799,999 | 7,600 | 1,700 | 9,300 | | |
| 800,000 | 899,999 | 7,600 | 1,750 | 9,350 | | |
| 900,000 | 1,000,000 | 7,600 | 1,776 | 9,376 | | |
| 1,000,001 | 3,000,000 | 7,600 | 1,875 | 9,475 | | |
| 3,000,001 | 5,000,000 | 9,500 | 2,000 | 11,500 | | |
| 5,000,001 | 10,000,000 | 9,500 | 2,000 | 11,500 | | |

BILA TOZO

TUMA PESA AIRTEL - AIRTEL

| Ada ya Airtel Money | Tozo ya Serikali | Jumla makato |
|---|---|---|
| 10 | - | 10 |
| 25 | - | 25 |
| 25 | - | 25 |
| 40 | - | 40 |
| 50 | - | 50 |
| 120 | - | 120 |
| 140 | - | 140 |
| 325 | - | 325 |
| 350 | - | 350 |
| 360 | - | 360 |
| 375 | - | 375 |
| 380 | - | 380 |
| 675 | - | 675 |
| 940 | - | 940 |
| 1,200 | - | 1,200 |
| 1,450 | - | 1,450 |
| 1,450 | - | 1,450 |
| 2,100 | - | 2,100 |
| 3,100 | - | 3,100 |
| 3,100 | - | 3,100 |
| 3,250 | - | 3,250 |
| 3,300 | - | 3,300 |
| 4,000 | - | 4,000 |
| 4,000 | - | 4,000 |
| 4,000 | - | 4,000 |

BILA TOZO

TUMA PESA MITANDAO MINGINE

| Ada ya Airtel Money | Tozo ya Serikali | Jumla Makato |
|---|---|---|
| 10 | - | 10 |
| 45 | - | 45 |
| 45 | - | 45 |
| 90 | - | 90 |
| 90 | - | 90 |
| 180 | - | 180 |
| 180 | - | 180 |
| 180 | - | 180 |
| 495 | - | 495 |
| 540 | - | 540 |
| 612 | - | 612 |
| 675 | - | 675 |
| 1,125 | - | 1,125 |
| 1,440 | - | 1,440 |
| 1,710 | - | 1,710 |
| 2,070 | - | 2,070 |
| 2,250 | - | 2,250 |
| 2,880 | - | 2,880 |
| 3,870 | - | 3,870 |
| 3,870 | - | 3,870 |
| 3,870 | - | 3,870 |
| 5,400 | - | 5,400 |
| 5,400 | - | 5,400 |
| 5,400 | - | 5,400 |
| 5,400 | - | 5,400 |

BILA TOZO

LIPA KWA AIRTEL MONEY

| Ada ya Airtel Money | Tozo ya Serikali | Jumla Makato |
|---|---|---|
| 20 | - | 20 |
| 50 | - | 50 |
| 70 | - | 70 |
| 100 | - | 100 |
| 200 | - | 200 |
| 300 | - | 300 |
| 500 | - | 500 |
| 500 | - | 500 |
| 850 | - | 850 |
| 920 | - | 920 |
| 1,000 | - | 1,000 |
| 1,200 | - | 1,200 |
| 1,700 | - | 1,700 |
| 2,000 | - | 2,000 |
| 2,600 | - | 2,600 |
| 3,000 | - | 3,000 |
| 3,300 | - | 3,300 |
| 4,500 | - | 4,500 |
| 5,500 | - | 5,500 |
| 5,700 | - | 5,700 |
| 6,000 | - | 6,000 |
| 6,000 | - | 6,000 |
| 6,000 | - | 6,000 |
| 6,000 | - | 6,000 |
| 6,000 | - | 6,000 |

BILA TOZO

FANYA MALIPO KWA AIRTEL MONEY

GePG MALIPO YA SERIKALI · LUKU · VING'AMUZI · MAJI · POLISI · SOLAR · BIDHAA MITANDAONI · MIAMALA YA KIBENKI · TRA · BRELLA · ARDHI · NDEGE · BIMA · VIKOBA · LIPA MITANDAO YOTE

2175704O2

Fanya yote na My Airtel App!
Pakua katika simu yako.

Download on the App Store · ANDROID APP ON Google play

Fanya malipo ya Serikali na bili mbalimbali kupitia My Airtel App

SUMATRA · Wizara ya Nishati na Madini · BRELA · Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi

KUMBUKA

Unaweza kuweka ama kupokea hadi Tsh 10,000,000 kwa siku na unaweza kutoa ama kutuma hadi Tsh 5,000,000 kwa siku kama usajili wako umekamilika na Airtel Money.

Kila mara unapotuma pesa, kumbuka kuhakiki namba ya mpokeaji kuepuka kukosea na usumbufu.

**Kuangalia salio Airtel Money ni BURE.**
Airtel Money huonesha salio kwenye kila muamala.
Kuangalia miamala miwili ya mwisho, taarifa ya muamala, muhtasari wa siku iliyopita, muhtasari wa siku, miamala ya mwezi uliopita, utatozwa gharama ya Tsh 50 kwa kila muamala.

Kuwasiliana na Huduma kwa Wateja, Piga 100 bure au tembelea duka lolote la Airtel Money Branch.

Agosti, 2023

HARAKA.SALAMA.BILA MIPAKA.

HABARI KITAIFA

# JWTZ yatoa siku saba kusalimisha mavazi ya kijeshi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

JESHI la Ulinzi la Wananchi Tanzania (JWTZ) limetoa siku saba kwa wananchi wote kusalimisha mavazi yanayofanana na sare zake.

Limeonya kuwa baada ya muda huo, litafanya msako mitaani na madukani, yeyote atakayebainika atachukuliwa hatua kali.

Kaimu Mkurugenzi wa Habari na Uhusiano Makao Makuu ya JWTZ, Luteni Kanali Gaudentius Ilonda, alitoa maagizo hayo jana jijini hapa alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu wimbi la baadhi ya wananchi kukamatwa wakiwa wamevaa mavazi hayo.

"Baada ya siku saba atakayekutwa nayo atachukuliwa hatua. JWTZ inaomba kupitia kwenu kuwafahamisha wananchi kuwa utekelezaji wa majukumu yake ya msingi na mengineyo unategemea sana ushirikiano mzuri na wananchi wote.

"Hivyo, uhusiano wa jeshi letu na wananchi ndiyo mhimili mkubwa ndani na nje ya nchi, siyo hekima kwetu kulumbana kwa namna yoyote ile na baadhi ya wananchi wenye mavazi yanayokatazwa," alisisitiza.

Luteni Kanali Ilonda alisema wametoa siku saba kuyasalimisha bila kuchukuliwa hatua ili kuepuka usumbufu na kwa ambaye hatafanya hivyo, atatafsiriwa kuwa na nia ovu.

"Baada ya siku hizo saba, vijana wetu wataingia mtaani na hakutakuwa na unyenyekevu huu ambao tunautumia leo kuomba wananchi kusalimisha mavazi haya katika kambi zetu na vituo vya polisi," alisema.

Akizungumzia hali ilivyo sasa, alisema kumekuwa na wimbi la baadhi ya wananchi wanaokamatwa au kuonekana wamevaa sare za JWTZ au mavazi yanayofanana na sare za kijeshi.

"Tumekutana hapa leo hii ili kupitia kwenu JWTZ liweze kutoa ufafanuzi kwa jamii ya Watanzania kuhusiana na kadhia hiyo inayokinzana na katazo la kisheria la raia kuvaa, kumiliki au kuuza mavazi ya kijeshi au yanayoelekea kufanana na sare za kijeshi," alisema.

Alikumbusha sheria inakataza kuvaa mavazi hayo ambayo ni pamoja na kombati, makoti, tisheti, suruali, magauni, kofia, viatu, mabegi na kaptula zenye rangi zinazofanana au kushonwa katika mitindo ya kijeshi.

"Katazo hili ni kwa mujibu wa Kifungu cha 99 cha Sheria ya Ulinzi wa Taifa (NDA) Sura ya 192, Sheria Namba 24 ya mwaka 1966 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2002. Kifungu cha 178 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 na kifungu cha sita cha Sheria ya Usalama wa Taifa, vinakataza raia kuvaa sare na mavazi ya majeshi ya ulinzi au yanayofanana nayo," alisema.

Alisema zipo baadhi ya taasisi zinazowashonea watumishi wake sare za aina hiyo, pia wapo wafanyabiashara wanaoingiza nchini mavazi ya aina hiyo na kuyauza kwa baadhi ya raia kupitia maduka au maeneo yao ya biashara.

"Aidha wapo baadhi ya wasanii wanaovaa mavazi hayo na kuyatumia wawapo katika majukwaa ya kazi zao bila kufuata utaratibu ambao ni kuomba kibali kwa ajili ya kuyatumia," alisema.

Kadhalika, alisema wapo baadhi ambao kwa kuyatumia mavazi hayo wamekuwa wakiwatapeli wananchi na wengine kufanya vitendo viovu ambao pia wamekuwa wakidhaniwa kuwa ni wanajeshi.

"Vitendo hivyo ni vya uvunjifu wa sheria za nchi hivyo havipaswi kufumbiwa macho aidha hali hii ikiachwa kuendelea inaweza kuhatarisha ulinzi na usalama wa nchi yetu" alisema.

Alisema JWTZ litaendelea kudumisha ushirikiano na mshikamno na wananchi ili kutimiza jukumu lake kwa mujibu wa Katiba ya nchi.


The Guardian Limited

JOB VACANCY

The Guardian Limited, **Publishers of leading Tanzanian newspapers, The Guardian, Nipashe and Nipashe Jumapili, is looking for motivated and experienced people to fill the position of:**

**SENIOR MARKETING EXECUTIVE – DAR ES SALAAM**

**Job Purpose:**

Developing and executing strategies to promote brands, products and services, maximizing profits for the company.

**Main Responsibilities:**

- Formulate an appropriate commercial strategy that responds to the overall development of the company's marketing operations, newspaper sales, advertisements and other printed products.
- Become knowledgeable expert of The Guardian Limited products and be experienced in identifying target markets and developing strategies to communicate with them.
- Identify, plan, prepare and produce proposals for the targeted audiences.
- Study competitors' products and services on a daily basis, with a view to designing counter strategies.
- Advise clients on their advertising and promotion campaigns.
- Organize all company events related to CSR, promotion, product launching, staff parties, etc.
- Monitor and analyze product performances, trends and provide accurate reports on programe and market information.
- Explore ways of improving existing products and services and increasing profitability.
- Advise the Management with feasibility studies on ways to get sponsorship for various events, highlighting benefits to the Company.
- Engage in negotiating and closing deals where and if appropriate.
- Prepare periodic performance reports for the Management and provide appropriate inputs towards improvement and the taking of remedial measures.
- Design and implement human resources training and development programme

**Minimum Qualifications and Experience:**

- University Degree in Business Administration/Sales & Marketing or equivalent.
- At least 5 years' relevant working experience.
- Excellent communication skills, computer knowledge and familiarity with a wide range of newspaper brands.

**MODE OF APPLICATION:**

Apply online via email address: **vacancy@guardian.co.tz** by **8th September, 2023.**

**NB:** Only shortlisted candidates will be contacted.

***Please note that The Guardian Limited is an equal opportunity employer.***


# TAKUKURU yamtaka mkandarasi kurudia mradi ujenzi wa barabara

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

TAASISI ya Kuzuia na kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Shinyanga, imemtaka mkandarasi, Kampuni ya Brampem Global Investment LTD, kurudia matengenezo ya barabara aliyojenga chini ya kiwango.

Pia imeagizwa mkandarasi huyo kukatwa fedha kutokana na kuchelewesha kukamilisha matengenezo hayo kinyume cha mkataba.

Mkandarasi huyo mbali na kuchelewesha Mradi huo, anadaiwa kutekeleza mradi chini ya kiwango kwa kutochonga barabara kwa usahihi, kina cha tabaka la kifusi kutofika kiwango na kutoshindiliwa ipasavyo pamoja na uchongaji wa mitaro isiyoridhisha.

Hayo yalibainishwa jana na Kaimu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Shinyanga, Mwamba Masanja, alipotoa taarifa kwa vyombo vya habari kuhusu utekelezaji wa majukumu ya taasisi hiyo kwa kipindi cha robo ya nne ya mwaka wa fedha 2022/2023.

Alisema kwa kipindi hicho walifanya ufuatiliaji wa miradi mbalimbali ikiwamo ya matengenezo ya barabara katika Manispaa ya Shinyanga chini ya usimamizi wa TARURA ili kuona utekelezaji wa miradi hiyo kama umezingatia ubora na viwango vinavyotakiwa.

Alieleza kuwa katika ufuatiliaji wa matengenezo ya barabara hizo - uboreshaji wa vipande vya barabara katika kata za Chamaguha, Ngokolo, Ndembezi, Kambarage na Mwasele, walibaini mkandarasi kutekeleza ujenzi wa barabara hizo chini ya kiwango.

Alisema kuwa mkandarasi huyo kwa sasa yuko katika kipindi cha makato ya fedha ikiwa ni adhabu ya kuchelewesha mradi kwa mujibu wa mkataba - alipaswa akamilishe mradi huo Aprili 27 mwaka huu, lakini licha ya kuongezewa siku 75, mradi haukukamilika.



# Madaktari bingwa wataja sababu ongezeko maradhi figo kwa vijana

**Na Mary Mosha,** MOSHI

DAKTARI Bingwa wa Magonjwa Yasiyoambukiza wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC, Dk. Elichilia Shao, amesema ongezeko la magonjwa ya figo, hasa kwa kundi la vijana, kunatokana na kutotibiwa ipasavyo magonjwa ya kisukari, shinikizo la damu na malaria.

Wakati wa kambi maalum ya uchunguzi wa magonjwa hayo iliyoratibiwa na Rotary Club Tanzania jana, Dk. Shao alisema idadi ya vijana wanaougua maradhi ya figo inaongezeka kwa wastani.

Dk. Shao alisema: "Kwa sasa tunaona vijana wanakuja figo ikiwa imefeli. Pamoja na kwamba kunachangiwa na haya magonjwa niliyoyataja. Bado tunaamini vyakula na vinywaji vikali vinachukua nafasi kubwa kwa vijana kupata maradhi ya figo.

"Kama wataalamu wabobezi, ni eneo la kuangalia kuona ni kwanini tunapata wagonjwa wengi zaidi, ambao ni vijana wenye umri mdogo?"

Alisema serikali ina kazi kubwa mbele yake kutoa elimu kwa jamii kuhusu matumizi sahihi ya vileo na unywaji wa pombe kali na dawa za asili ambazo watu wanatumia ilhali hazijathibitishwa ubora.

"Ni muhimu sana watafiti wakaanza utafiti kubaini visababishi vingine vya magonjwa haya hasa kwa vijana, maana hawa ndio tunaowategemea kufanya kazi.

Maana yake, wakiwa wengi tutakuwa na taifa la wagonjwa na tutashindwa kufikia maendeleo tunayoyataka," alitahadharisha.

Alifafanua zaidi kuhusu suala hilo, Dk. Jojet Josephat, alisema ongezeko hilo la wagonjwa wa figo, hasa vijana, linachagizwa na imani potofu kwamba magonjwa yasiyoambukiza kama figo huwapata watu wenye umri mkubwa.

"Vijana tubadilishe mfumo wa maisha, tufanye mazoezi na tuepuke unywaji wa pombe kupitiliza. Pia tujitokeze mara kwa mara kupima afya," alisisitiza.

Mratibu Mwenza wa Kambi hiyo ya uchunguzi, Young Kimaro, alisema Rotary imeandaa kambi hiyo ili watu wapime afya zao na kuokoa maisha yao kwa kupata tiba kwa wale watakaogundulika.

"Kambi hii ni ya bure kwa watu wote ambapo elimu inayotolewa ni pamoja na ile itakayowasaidia watu kubaini dalili za maradhi yasiyoambukiza, jinsi ya kujikinga nayo na pia kukabiliana nayo pale yanapoibuka.

"Kambi hii ni sehemu ya programu maalum ya Rotary Tanzania kwa ushirikiano na Rotary International inayolenga kutoa huduma kwa jamii yenye uhitaji," alisema Mratibu wa Kitaifa wa Kambi hiyo, Harish Bhatt.



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga (watatu kushoto) na Mkuu wa Wilaya ya Babati, Lazaro Twange (watatu kulia) wakifurahia kwa makofi na wanafunzi wa shule ya sekondari Sigino baada ya kuzindua madarasa mapya juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wanafunzi sekondari wapatiwa kompyuta

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

SHIRIKA la Camara Education Tanzania limetoa msaada wa Kompyuta 100 zenye thamani ya Sh. milioni 37 kwa shule nne za sekondari za mikoa ya Tanga na Pwani.

Kila shule itanufaika kwa kupata kompyuta 25 zitakazowezesha wanafunzi kujifunza masomo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Mkuu wa Wilaya ya Korogwe, mkoani Tanga, Jokate Mwegelo, alisema jana kuwa msaada huo umetolewa na Shirika la Camara Education Tanzania kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) yenye jukumu la kisheria la kukusanya michango kwa ajili ya sekta ya elimu nchini.

Kabla ya kukabidhi kompyuta hizo kwa Shule ya Sekondari Semkiwa, Jokate aliwahimiza wanafunzi kusoma kwa bidii kutokana na kuwekewa mazingira mazuri ya kujifunza na kufundisha.

"Namna pekee mnayoweza kuonyesha shukrani kwa wafadhili walioleta msaada shuleni kwenu ni kusoma kwa bidii na kuendelea kufanya vizuri katika masomo yenu," alisema.

Mkuu wa Wilaya huyo alikabidhi kompyuta hizo kwa Shule ya Sekondari Semkiwa iliyoko Halmashauri ya Mji wa Korogwe na Shule ya Sekondari Kwaluguru ya Halmashauri ya Wilaya ya Handeni.

Katika Mkoa wa Pwani, shule zitakazonufaika ni Shule ya Sekondari Rafsanjani Soga iliyoko Halmashauri ya Mji Kibaha na Shule ya Sekondari Simbani iliyoko Halmashauri ya Kibaha.

Kabla ya makabidhiano hayo, Mwakilishi wa Camara Education Tanzania, Asia Bonanga, alisema Shirika la Camara Education Tanzania, limedhamiria kupeleka teknolojia ya mawasiliano shuleni ili kusaidia jitihada za kupatikana elimu bora nchini.

Kwa mujibu wa Bonanga, maono ya Camara Education Tanzania ni kuhakikisha hakuna mwanafunzi anayeachwa nyuma katika TEHAMA.

Kaimu Mkurugenzi wa Miradi na Utafutaji Raslimali na Usimamizi wa Miradi kutoka TEA, Masozi Nyirenda, alishukuru Shirika la Camara Education Tanzania kwa msaada huo wa kompyuta na kukumbusha shule zilizonufaika, kuzitumia na kuzitunza vizuri ili zidumu na kunufaisha kundi kubwa la wanafunzi.

"Kama tunavyofahamu, vifaa hivi vinahitaji utunzaji maalum ikiwa ni pamoja na kuwa na vyumba vinavyofaa, hivyo shule nufaika zijiandae vyema kwa hili," alisema Nyirenda.

TEA ni Taasisi ya umma inayofanya kazi chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa, taasisi hiyo inafadhili ujenzi wa miundombinu ya elimu ikiwamo madarasa, nyumba za walimu na matundu ya vyoo.

Mfuko huo umekuwa ukijenga, mabweni, mabwalo na majiko yake, maabara na upatikanaji wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia katika ngazi zote za elimu Tanzania Bara na ngazi ya Elimu ya Juu kwa Tanzania Zanzibar.

# Waliohamishwa Ngorongoro wasimulia mwaka mmoja wa maisha ya Msomera

**Na Mwandishi Wetu,** HANDENI

WAKAZI wa Kijiji cha Msomera, wilayani Handeni mkoani Tanga, wamesema kuhamia katika eneo hilo kumewapa nafasi ya kujifunza shughuli za kilimo tofauti na walivyokuwa wamezoea kufuga.

Katika mazungumzo na mwandishi wa habari hizi jana kijijini huko, wananchi hao walisema ni mwaka mmoja tangu kuhamia Msomera na kuanza kulima. Hali ya hewa ni nzuri, sasa wanavuna mahindi na maharagwe.

Mchungaji Peter Kitui alisema moja ya fursa ambayo walikuwa wanaikosa ni kujihusisha na shughuli za kilimo, Walitegemea zaidi kufuga, lakini wanaamini kwa maisha ya kawaida mtu lazima afanye shughuli zaidi ya moja.

Alisema kwa hatua za awali, ameshalima ekari tatu za mahindi, akifanya kilimo mseto kwa kuchanganya na maharagwe na alizeti, mazao ambayo kwa Msomera yanastawi.

Diwani kutoka Ngorongoro, Joanes Tiamas, aliomba maofisa wa kilimo kuendelea kuwatembelea mara kwa mara kuwapatia elimu ya kilimo.


"Kule asili yetu ilikuwa ni ufugaji tu, hakuna rukhsa ya kulima, hivyo wengi wetu kama wafugaji tulikuwa tunategemea mifugo katika maisha yetu. Hili suala la kulima ni jipya lakini tuna imani litabadili maisha yetu," alisema Tiamas.

Naibu Kamishna Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro (NCAA), Elibariki Bajuta, alieleza sababu ya serikali kuwapeleka wananchi hao Msomera ni baada ya kubaini eneo hilo shughuli za ufugaji na kilimo zinawezekana.

Alisema wataalamu wa masuala ya ardhi walipita katika maeneo hayo na kuona kuna rutuba na wananchi wanaweza kulima mazao mbalimbali, pia kuendelea na ufugaji kama Ngorongoro.

Naye Moi Molel alisema mbali na fursa za kilimo, pia wananufaika na biashara mbalimbali ikiwamo kuendesha pikipiki za kubeba abiria, maarufu bodaboda.

Wananchi hao kutoka Ngorongoro wametimiza mwaka mmoja katika Kijiji cha Msomera tangu kuhamishiwa huko.





# Serikali yaweka mikakati kudhibiti ujangili

**Na Neema Charles,** SAUT

SERIKALI kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii, imesema tatizo la ujangili na biashara haramu ya nyara za wanyamapori na mazao ya misitu imeendelea kuwa tatizo na kudumaza uchumi wa nchi na kuhitaji ushirikiano dhidi ya vita hiyo.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori nchini, Kiza Baraga, wakati wa kuwajengea uwezo viongozi na watendaji wa vikundi vya uratibu wa doria kanda za kiikolojia (TCGs) dhidi ya ujangili na biashara haramu ya wanyamapori.

Alisema moja ya mikakati waliyoiweka ni pamoja na kushirikisha jamii li kudhibiti mitandao ya ujangili na usafirishaji haramu wa nyara za serikali ambayo hupangwa nje ya hifadhi na kutekelezwa ndani ya maeneo hayo.

"Kufuatia hatua hiyo, serikali imeanza kuzijengea uwezo mpana taasisi na jamii mbalimbali zinazohusika katika kukabiliana na ujangili na biashara haramu ya wanyamapori na mazao ya misitu katika maeneo mbalimbali nchini ili kuhakikisha majangili wanakamatwa kabla hawajatekeleza adhma yao," alisema Baraga.

Meneja wa Mradi wa kupambana na Ujangili na Biashara Haramu ya Nyara za Wanyamapori. (IWT- Project), Theotimos Rwegasira, alisema katika kukabiliana na ujangili nchini serikali ilizindua Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Ujangili nchini (2014-2019) kwa lengo la kudhibiti ujangili.

Warsha hiyo iliandaliwa na Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Mradi wa IWT. Ikiwa ni muendelezo wa mpango wa kuzijengea uwezo Taasisi za kisheria ili kukabiriana na ujangili nchini hususani kikosi kazi cha Taifa cha kupambana na ujangili (NTAP) na Kanda za Kiikolojia za uratibu wa doria (TCG's).

# Hali ya watumishi kupata uzito uliopitiliza yashtusha

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WATUMISHI 20 kati ya 60 wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela iliyopo mkoani Mwanza wamekutwa na uzito uliopitiliza baada ya kupimwa hali zao za lishe sawa na asilimia 33.3 ya watumishi hao huku wakihimizwa kufanya mazoezi na kuhakikisha wanakula vyakula stahiki na kwa wakati unaotakiwa ili kurejesha afya zao katika hali za kawaida.

Akizungumza baada ya watumishi hao kufanyiwa vipimo vilivyoratibiwa na idara ya lishe ya manispaa hiyo iliyoenda sambamba na upimaji wa presha na kutoa elimu ya lishe bora, Ofisa Lishe wa Manispaa ya Ilemela, Pili Kassim, aliwakumbusha kuwa na namna nzuri ya ulaji kwa ajili ya afya zao.

Aliwataka watumishi hao kujenga tabia ya kupima hali zao za lishe mara kwa mara, kuzingatia ulaji unaofaa pamoja na kufanya mazoezi kwa kufanya hivyo kutawaepusha magonjwa yakiwamo ya kisukari, magonjwa ya moyo na utapiamlo.

Alisema idara ya afya imeona kuna haja ya kupima hali ya lishe kwa watumishi kwa kuwa wengi wao hawana muda wa kufuatilia hali za lishe kutokana na majukumu mengi walionayo na kuwaletea huduma hiyo karibu.

"Utaratibu huu utaendelea hadi kwa watumishi wa ngazi za chini kwenye kata na mitaa ambako ngazi ya halmashauri, utaratibu huo utakuwa endelevu kwa kila robo ya mwaka na kwa watumishi waliopo ngazi za chini itakuwa mara mbili kwa mwaka," alisema Kassim.

Naye Mkuu wa Idara ya Lishe Joyce Albert, alisema kuwa upo umuhimu wa kuendelea kutoa elimu ya lishe kwa watumishi na wananchi ili kuimarisha hali zao za afya. "Vipimo tulivyowafanyia watumishi vimedhihirisha kuwa idadi ya wenye uzito uliopitiliza ni kubwa sana hali inayoweza kupunguza ufanisi wa kazi kadhalika tuwatake sasa kujitokeza mara kwa mara kupima hali zao ili kuona namna ya kuweka afya zao imara," alisema Albert.

Mtumishi kutoka Divisheni ya Utawala upande wa utunzaji wa kumbukumbu, Chami Sollo, alisema kuwa amepata elimu ya namna bora ya kuzingatia ulaji wa vyakula na kufanya mazoezi kitendo ambacho kitawakinga dhidi ya magonjwa.




Mwenyekiti wa Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, Gagi Lala akizungumza na madiwani wake (hawapo pichani) wakati wa kikao cha baraza la madiwani cha robo ya nne ya mwaka wa fedha 2022/2023 cha kujadili masuala mbalimbali ya maendeleo, kulia kwake ni Makamu Mwenyekiti wake Doa Limbu na Katibu wa Siasa na Uenezi CCM Wilaya ya Kahama, Joakimu Simbira na kushoto ni Mkurugenzi wa Halmashauri, Hadija Kabojela juzi. **PICHA; SHABAN NJIA.**

# Hospitali, zahanati zakosa wataalamu maabara

**Na Daniel Limbe,** BIHARAMULO

HALMASHAURI ya Wilaya ya Biharamulo imetajwa kuwa na uhaba wa wataalamu wa maabara kwa kuwa na wataalamu tisa pekee wanaohudumia katika hospitali, vituo vya afya na baadhi ya zahanati huku hospitali ya wilaya hiyo pamoja na zahanati 16, zikikosa wataalamu hao na kuzorotesha hali ya utolewaji wa huduma wilayani humo. Wataalamu hao tisa wanahudumia katika maeneo yenye uhitaji mkubwa na idadi yao kwenye mabano ambazo ni pamoja na Hospitali teule ya Biharamulo (2), Kituo cha Afya Nyakanazi (1), Kituo cha Afya Kalenge (1), Kituo cha Afya Nemba (1), Kituo cha Afya Nyabusozi (1), Zahanati ya Luganzu (1), Zahanati ya Nyantakara (1) na Zahanati ya Kikomakoma (1) huku hospitali ya wilaya pamoja na zahanati 16 zikikosa wataalamu hao.

Hayo yamebainishwa na Kaimu Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Benedictor Marwa, baada ya baadhi ya madiwani wa halmashauri hiyo kulalamikia ukosefu wa watalaamu hao na kuwa kati ya maeneo hayo ambayo yana uhaba wa wataalamu hao ni hospitali ya wilaya pekee yenye wataalamu wanaojitolea kutoka taasisi ya Benjamin Mkapa.

Alisema, mgawanyo wa wataalamu hao unategemea ukubwa wa mahitaji ya vituo vya kutolea tiba huku akiwashauri madiwani hao kushirikiana na wakuu wa vituo vya kutolea huduma za tiba kuajiri wataalamu husika na kuwalipa kupitia makusanyo ya vituo hivyo wakati wakisubiri ajira rasmi za serikali.

Kadhalika, katika zahanati 16 ambazo hazina kabisa wataalamu, huduma za uchunguzi wa magonjwa zinazotolewa ni zile za awali huku wagonjwa wanaohitaji uchunguzi mkubwa huagizwa kwenda vituo vya afya ambavyo vinawataalamu hao.

Adha hiyo iliibuliwa na Diwani wa Kata ya Kalenge, Erick Method, wakati akiwasilisha taarifa za maendeleo ya kata yake kwenye kikao cha baraza la madiwani hao, jambo ambalo limeendelea kuonekana kuwa kero kwa kata mbalimbali.

Kutokana na hali hiyo, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Leo Rushahu, aliunga mkono kauli ya Mganga Mkuu wa wilaya kuwataka madiwani kushirikiana na Wakuu wa Vituo vya kutolea huduma za afya kuajiri wataalamu hao kwa mikataba ya muda ili kusaidia kupata tiba sahihi kwa magonjwa yanayo wasibu wananchi.

"Nielekeze tu kuwa madiwani tushirikiane na wataalamu wetu kutatua adha hiyo kwani tuna baadhi ya vyanzo vyetu vya mapato kutoka kwenye Vijiji na hata kwenye Kata zetu vitusaidie kuajiri wataalamu hao ikiwa ni pamoja na gharama za uchangiaji wa matibabu kwa jamii," alisema Rushahu.



Ukurasa 12

Ubunifu PPP kiwandani na kwa wakulima malighafi yao, yaja na neema hadi serikalini




Ukurasa 13

Huu ndio wakati muziki wa Singeli kutawala sanaa yetu

BUFE

IJUMAA AGOSTI 25, 2023

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Ukurasa 14

**TARI MAKUTUPORA:**

**Tumetimiza kivitendo agizo la Majaliwa, kubuni mbegu ya zabibu yenye tija kitaifa**

UCHUMI

SAFARI YA MAENDELEO AWAMU SITA

# Simulizi Rais Dk. Samia anavyosimamia mageuzi kwenye PPP na uwekezaji wake

**Na Peter Orwa**

***JANA katika ukurasa kama huu, kulikuwa na simulizi namna Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, anavyozungumza lugha moja na wana- dini katika eneo la mazingira nchini. Leo, fuatilia kwenye uchumi, biashara na uwekezaji, hasa Sera ya Ubia wa Serikali na Sekta Binafsi- PPP. Endelea...***



Shughuli za uzalishaji kiwandani zikiendelea, eneo mojawapo ambalo Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, anapigania uwekezaji uongezeke, kupitia sera ya PPP. **PICHA: MTANDAO**

WAKATI serikali inazingatia katika uongozi awamu ya nne, ikafika uamuzi wa kuendesha rasmi kilichoanzishwa katika awamu ya pili, mageuzi kuelekea sekta binafsi chini ya Rais Ali Hassan Mwinyi, aliyerithi uongozi wa nchi kutoka mfumo hodhi kiuchumi wa wakati huo uliodumu kwa miaka 21 nchini, pia kupata mwendelezo wa maboresho yake, kutoka kwa hayati Rais Benjamin Mkapa.

Katika zama awamu ya nne, kukaanzishwa mambo makuu mawili, sera na sheria inayohusu ubia wa sekta binafsi katika kuinua uzalishaji, maarufu PPP.

Ubia huo ndio unaojenga zaidi uwekezaji rasmi kisheria na kisera wa sekta binafsi katika biashara na huduma nchini.

Rais Dk. Samia anaweka wazi kwamba, katika kufanikisha maendeleo ya nchi, nafasi ya sekta binafsi haikwepeki, bali ni mbia wa kudumu.

Hilo anaungwa mkono na mtendaji wake mwandamizi kiserikali, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Lawrence Mafuru, mnamo Machi mwaka huu anaposema serikali inafanya majadiliano ya kimkakati na Benki ya Dunia, kuiwezesha sekta binafsi kushiriki katika miradi ya maendeleo kupitia PPP.

Hilo ni tamko, baada ya kufanya mazungumzo na ujumbe wa Benki ya Dunia, iliyoongozwa na Mkurugenzi Mkazi wake nchini, Nathan Belete, wakijadili namna bora ya utekelezaji PPP na uboreshaji mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara nchini.

Balete anasema majadiliano hayo ni utekelezaji wa msisitizo na maelekezo yanayotolewa na Dk. Samia Suluhu Hassan, kwamba sasa ni wakati wa hatua zaidi ya sekta binafsi kushirikiana na serikali, kwa ajili ya kuleta maendeleo ya kiuchumi.

Anarejea Rais Dk. Samia anachosisitiza kwao kila wakati, kwamba sekta binafsi inapoweza kufanya jambo fulani, hakuna haja ya kutumia fedha za serikali kwa eneo hilo, ila changamoto iliyopo ni namna mfumo unaweza kusaidia miradi kufanyika kwa njia ya PPP.

"Wenzetu wa Benki ya Dunia wamekuwa mstari wa mbele katika kutoa fedha sio tu katika miradi ya kijamii, lakini sasa wanajielekeza zaidi kutoa fedha na misaada ya kitaalamu kuhakikisha kwamba eneo hili la PPP, sambamba na uboreshaji mazingira ya uwekezaji na biashara nchini yanafanikiwa," anasema Mafuru.

Akasema kwa sasa serikali imeshaanza majadiliano ya awamu ya pili na Benki ya Dunia kuhusu msaada unaojielekeza kwenye sekta za miundombinu, kuboresha mazingira ya kufanyika biashara nchini.

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu huyo, Sheria ya Ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP) inafanyiwa marekebisho, ili iweze kuwa na ushindani, kuvutia mitaji ya sekta binafsi na hatimaye kuwezekana kushirikiana na serikali katika kutekeleza miradi kitaifa.

Anaitaja kuwa ni hatua itakayopunguzia serikali mzigo wa kibajeti kwenye miradi ambayo inaweza kufanywa na sekta binafsi

Jumatatu wiki hii, akizungumza kwenye hafla ya miaka 60 ya kuwapo Kanisa la Kiinjili ya Kilutheri Tanzania (KKT), Mkuu wa kanisa hilo, Askofu Fredrick Shoo akamhakikishia Rais Dk. Samia, kwamba wao kanisa wako mstari wa mbele kushirikiana na serikali kutekeleza PPP nchini humo.

Askofu Dk. Shoo anasisitiza wao kuwekewa mazingira rafiki katika utekelezaji wake PPP na wadau wengine, hata kuwa na sura rafiki jambo ambalo Rais Dk. Samia akaliafiki kwa msisitizo.

Katika hilo, mkuu huyo wa nchi, anatoa historia namna amekuwa akiteta na viongozi wa kidini, kama sehemu ya wao serikali wanafikia uamuzi wa mambo makuu kadhaa ya kitaifa.

Katika moja ya maendeleo ya nchi kupitia PPP, Rais Dk. Samia akashiriki uzinduzi katika shughuli za maboresho ya kitaaluma, katika Chuo Kikuu cha Makumira cha Arusha, kilicho chini ya KKKT, ambayo ni sura ya PPP katika ngazi ya huduma ya elimu.

Kwa mujibu wa Waziri wa Viwanda na Biashara, Ashatu Kijaji, idadi ya wawekezaji kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Machi, 2021 mpaka mwezi Februari mwaka jana, serikali imefanikiwa kuvutia na kupitia kituo cha Uwekezaji (TIC,) jumla ya miradi 294 yenye thamani ya shilingi trilioni 118.75 imesajiliwa na ikatarajiwa kutoa jumla ya ajira rasmi zaidi ya 62,000 kwa Watanzania.

### UJIO SEKTA BINAFSI

Kimsingi, ujio wa sekta binafsi unaondelea sasa nchini, umepitia hatua kadhaa katika mageuzi yaliyohamisha nchi kutoka mfumo huria kiuchumi mwaka 1985 na baadaye kisiasa mwaka 1992, kurejea kilichokuwapo baada ya uhuru hadi mwaka 1964, Ni mageuzi aliyoanza nayo Rais Ali Hassan Mwinyi.

INAENDELEA UK.12

UCHUMI

# Ubunifu wa PPP kiwandani na kwa wakulima malighafi yao, yaja na neema hadi serikalini

• Mapato ya wote juu, kilimo nacho chapaa kitaifa; ubia wa hoja ya Rais inavyotekelezwa shambani

**Na Frank Monyo**

SEKTA ya Kilimo hadi sasa kihistoria ni mhimili wa maendeleo ya uchumi Tanzania. Ni sekta inayotajwa kuchangia nusu ya Pato la Taifa, na robo tatu ya bidhaa zinazouzwa nje ya nchi.

Vilevile, ndiko penye chanzo cha chakula, pamoja na utoaji fursa za ajira zaidi ya asilimia 75 ya Watanzania.

Kilimo kinatajwa kuwa na uhusiano na sekta zisizo kuwa za kilimo, kupitia usafirishaji kwenda kwenye usindikaji wa mazao ya kilimo, matumizi na uuzaji nchi za nje. Ni sekta inayotajwa kutoa malighafi kwa viwanda na soko linalotawala.

Tanzania hadi sasa inazalisha takribani asilimia 97 ya mahitaji yake ya chakula. Lakini, uzalishaji mazao unatofautiana mwaka hadi mwaka, kutegemea na kiasi cha mvua kilichopatikana.

Maboresho ya kiuchumi yanayoendelea sasa yamesababisha kufunguka sekta hiyo kwa uwekezaji binafsi katika uzalishaji na usindikaji, uagizaji pembejeo za kutoka nchi za nje na usambazaji na masoko ya kilimo. Serikali imebaki na kazi ya usimamizi na usaidizi wa umma na dhima ya uwezeshaji.

Kilimo kama ilivyo katika sekta nyinginezo za uzalishaji huduma na bidhaa, serikali inaungana na sekta binfasi kupitia ubia wa serikali, unaiota kisera na kisheria -PPP. Vilevile, mifumo ya uwekezaji kisera ina wajibu wa kurejesha matunda ya uzalishaji wake kwa umma jirani, kupitia sera ya uwekezaji, ambayo nayo ni sehemu ya PPP.

### PPP YA WAKULIMA, KIWANDA MFADHILI

Hapo ndipo sekta binafsi, Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL), inaungana na serikali kuongeza thamani katika shughuli za kilimo kwa wakulima wadogo, ikianzisha kilimo cha mkataba.

Kwa sasa kampuni hiyo inashirikiana na wakulima wadogo kutoka mikoa saba, kupitia mpango wao wa kutoka kwenye nafaka mpaka kwenye mafanikio ya juu.

Ni kupitia mkataba huo, wamekuwa wakishirikiana na wataalamu wa kilimo, wakiwajengea ujuzi wakulima hao na kuwapatia pembejeo muhimu, ili waweze kuzalisha nafaka za kutosha na zenye viwango vinavyotakiwa.

Kijografia, ardhi ya kilimo Tanzania hadi sasa inakadiriwa kuwa wastani wa hekari 3,502,500 kwa mujibu wa taarifa ya Benki ya Dunia ya mwaka 2020.

Hiyo inabeba maana kwamba, endapo miundombinu sahihi itawekwa mahali hapo, bahati ya wakulima wengi na sekta ya kilimo kwa ujumla inaweza kubadilika na kuchangia zaidi ya asilimia 27 ya Pato la Taifa, ambayo inachangia kwa sasa.



Sehemu ya shughuli za kilimo zinazosimamiwa na Kiwanda cha Bia Serengeti, katika ubia wake na wakulima ikiwainua katika tija shambani.
**PICHA: MAKTABA**

> **Kupitia vipindi vya mafunzo na warsha, tumejifunza mbinu rafiki kwa mazingira, kama vile kuchagua njia bora zinazohifadhi mazingira kama vile umwagiliaji badala ya kuharibu hifadhi zetu muhimu za maji.**

Meneja wa Mawasiliano na Uendelevu wa kampuni ya Serengeti, Rispa Hatib, anasema chanzo kikuu cha malighafi zinazotumika katika uzalishaji katika kampuni yao kinatokana na mazao ya kilimo, hivyo wamekuwa wakifanya kazi kwa karibu katika ushirikiano na wakulima wadogo wa ndani, ili kupata malighafi kutoka kwao.

"Wakulima wadogo wana matumaini kuhusu mabadiliko yanayoendelea katika sekta ya kilimo. Katikati ya mabadiliko hayo, sisi tumejikita kuhakikisha kilimo kinawanufaisha wakulima kupitia mpango wetu wa kilimo-biashara," anasema Rispa.

Katika kilele cha Sikukuu ya Wakulima na Wafugaji maarufu Nanenane yaliofanyika kitaifa mkoani Mbeya, serikali ilionyesha dira katika sekta ya kilimo, kwa kueleza mipango itakayowanufaisha wakulima wadogo, wa kati na wakubwa katika shughuli zao za uzalishaji.

### NAFASI YA RAIS

Rais Samia Suluhu Hassan, akihitimisha maonyesho hayo, alizindua programu ya uchimbaji wa visima kwa ajili ya wakulima wadogo 67,850 kwa nchi nzima itakayowezesha jumla ya ekari 2,7014,000 kufikiwa na mfumo wa umwagiliaji.

Akitoa maelezo kwa Rais Samia katika maonesho hayo kwenye viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya, Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe akafafanua kila kisima kitakuwa na uwezo wa kuhudumia wakulima 16.

Akaongeza kuwa kisima hicho kitakuwa na tanki zenye lita 5000 litakalokuwa limefungwa mfumo wa umeme jua (solar panel) kwa ajili ya kuisukuma.

"Pia mkulima atapewa eneo la umwagiliaji la heka 2.5 na mkulima wa kwanza katika programu hii anatoka wilayani Mbarali mkoani Mbeya," anasema.

Mpango huo unaenda sambamba na ule wa SBL, wa kuwawezesha wakulima wadogo kuzalisha mazao bora kwa ajili ya matumizi ya uzalishaji wa viwanda vya kampuni hiyo.

### RAI YA WAKULIMA

Katika maonyesho hayo, Bora Masaki, ambaye ni mkulima mdogo, anatumia nafasi hiyo kuipongeza kampuni hiyo kwa mchango wao kwenye sekta ya killimo, inapowawezesha wakulima kutoa malighafi nzuri.

"Kupitia mkakati wa kilimo-biashara, SBL imebadilisha hatma za wakulima wadogo wadogo. Tuliokolewa na SBL kupitia mfumo wao wa msingi wa kilimo cha mkataba na sasa tunauhakika wa kuzalisha mazao yetu na uhakika wa soko," anatamka na kuongeza:

"Walitathmini kwa kina ubora wa shayiri yetu na kukiri uwezo wake kwenye uzalishaji. Tangu wakati huo, SBL imesimama upande wetu kama mshirika anayetegemewa na kutoa soko thabiti kwa mavuno yetu ya kilimo."

Masaki anasema, suala la ukosefu wa masoko kwa sasa, linakuwa la uhakika, kutokana na kuwapo ushirikiano na SBL.

"Wakulima sasa wanapata malipo thabiti na uhakika wa kupata usaidizi wa kifedha kutoka kwa taasisi za fedha ili kuwekeza tena katika ubia wao wa kilimo. Hii inawakilisha mageuzi ya kilimo, yanayochochewa na uungwaji mkono thabiti wa SBL," anasema.

Thomas Venance, mkulima kutoka mkoani Kilimanjaro, anasimama kama kielelezo cha mchango wa kilimo cha mkataba kinachoongozwa na SBL, akiwa ana simulizi:

"Kwa muda wa miaka saba tu katika ushirikiano wangu na kampuni hii, nimeweza kupanua ardhi yangu ya kilimo kutoka hekari 50 hadi 100." Pia, anatamka matarajio yake makubwa maradufu katika siku zijazo.

Anaeleza kuwa SBL imewapatia ziada ya mbegu bora za shayiri kwa msimu uliopo wa kilimo, ikitarajiwa kuwepo ongezeko la asilimia 20 katika pato lijalo la mavuno yao.

Constansia Mghamba, mke na mama watoto wanne kutoka Moshi, mkoani Kilmanjaro, naye anaangukia kwenye orodha ya kufurahia mkakati wa kilimo cha mkataba wa SBL.

"Mpango huu wa kimapinduzi unawapa wakulima wadogo rasilimali muhimu za kilimo, kama vile mbegu bora, mbolea, mwongozo wa kitaalam na mafunzo, yote bila gharama yoyote," anasema Constansia.

Pia, anafafanua kuwa SBL ina mpango kama ule wa serikali wa kujenga visima vinavyowezesha umwagiliaji na kuwahakikishia wakulima kupata maji kwa uhakika.

Mwinyi Makame, mkulima kutoka Manyara mkoani Arusha, anaeleza thamani ya maarifa aliyopata wakati wa safari hiyo ya ushirikiano inavyomsaidia kukabiliana na changamoto kwenye kilimo.

"Kushirikiana na SBL imekuwa safari ya kipekee yenye kujenga uvumilivu, uthabiti na ukakamavu na kuleta tija katika shughuli zangu za kilimo," anasema Mwinyi na kuongeza:

"Kila msimu wa upanuzi hutuletea changamoto, lakini kwa kuungwa mkono na SBL, tumepata uwezo wa kuvuka changamoto hizi kwa uhakika mpya.

"Kupitia vipindi vya mafunzo na warsha, tumejifunza mbinu rafiki kwa mazingira, kama vile kuchagua njia bora zinazohifadhi mazingira kama vile umwagiliaji badala ya kuharibu hifadhi zetu muhimu za maji".

Anasema kuwa kilimo cha mkataba kinaenda sambamba na juhudi za serikali za kuhakikisha wakulima wanapata masoko yanayostawi, bei nzuri na za uhakika na kupunguza hasara baada ya mavuno.

"Kimekuwa sehemu muhimu ya kilimo nchini Tanzania, huku kikileta suluhisho kwa vikwazo vinavyowakabili wakulima" anatamka Mwinyi na kuendelea:

"(Killimo) iwe inahusu kuhakikisha uwepo wa rasilimali muhimu za kilimo au kurahisisha kuingia kwa taasisi za kifedha ili kukuza pato, mbinu hii ya ubunifu ya SBL imefungua njia kuelekea ustawi wa kustahimili kwa jamii za vijijini."

## Simulizi ya Dk. Samia anakosimama na mageuzi kwenye PPP

**INATOKA UK.11**

Hatua hiyo, ikaendana na mabadiliko makubwa ya kisera na kisheria zaidi, hasa mwanzoni mwa miaka ya 1990 na hata ilipofika katika awamu ya tatu ya uongozi kuanzia mwaka 1995, kwa miaka 10 kukashuhudiwa mengi ya mageuzi kusonga katika sura huria.

Moja kuu, ni kuhitimisha matatizo ya mabadiliko ya kisheria na kisera, serikali chini ya Rais Mkapa, ikaahidi mageuzi makubwa ikiwamo serikali kuhamia zaidi katika uratibu na usimamizi wa umma, uzalishaji na hata biashara, zaidi ukibaki katika sekta ya umma.

Tayari, Sheria ya Mashirika ya Umma iliyotawala nchini tangu mwaka 1969, maarufu SCOPO, ikafanyiwa mabadiliko mwaka 1992 kuendana zaidi na mahitaji mapya katika mageuzi tajwa, hasa yabaki katika yale yanayohudumia kibiashara zaidi.

Pia, kwa awamu ya tatu ya uongozi wa nchi, mwaka 1996 hadi 2005, ikapigwa hatua zaidi ya kuundwa Tume ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (PSRC), ikibeba jukumu la mageuzi kuhamisha asasi hizo, kuwa na sura ya sekta binafsi.

Kwa mujibu wa mageuzi hayo, kuna mashirika yenye hali mbaya zaidi yakabinafsishwa kwa asilimia zote; mengine yenye nafuu yakabinafsishwa kwa kuuzwa kwa wananchi, wawekezaji binafsi, pia kuna hisa zikabaki serikalini.

Hapo ndipo zinapatikana taasisi kama benki ya NMB, yenye mzizi kutoka iliyokuwa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), serikali hadi sasa ikiwa na sehemu ya mtaji wake.

Vilevile, kuna taasisi za umma ambazo ubinafsishaji wake ukafanyika kwa kukodishwa kwa muda maalum (wastani miaka 20), kisha hisa zinarudishwa kwa mmiliki wa awali, mfano hai ni kwenye Shirika la Reli Tanzania (TRC).

Hata hivyo ubinafsishaji wa TRC kwa kampuni ya India ukaingia dosari katika utekelezaji, hata mkataba kuvunjwa na hisa zikarejeshwa serikalini.


Pia, aina ya mwisho ya ubinafsishaji ukagusa hisa kuuzwa kwa wafanyakazi wa taasisi husika, maarufu kwa jina la MEBO (Management by Ownership), hapo nako kukiwapo mfano hai kwa Kiwanda cha Uchapaji cha Taifa (KIUTA), cha Dar es Salaam, ambacho kinafanya kazi hadi sasa.

Ni bahati mbaya sehemu kubwa ya mageuzi hayo yaliyofanywa chini ya PSRC, hayakufikia tija kubwa, jambo ambalo katika sura kuu inamsukuma Rais Dk. Samia katika juhudi kurejesha kiwango kikubwa cha uwekezaji miradi nchini na hasa katika eneo la uzalishaji kabla ya mageuzi, azma iliyoanza kukusudiwa na PSRC.

Hadi sasa tija inaonekana katika zama za awamu ya sita ya uongozi wa nchi, uzalishaji wa moja kwa moja, hadi huduma kimaendeleo nchini ziko dhahiri, kwa namna miradi mbalimbali ya uzalishaji na huduma iliendelea kuenea, mfano hai wa maboresho hayo kielimu ni matukio ya uzinduzi kwenye Chuo Kikuu cha Makumira, mkoani Arusha, mapema wiki hii chini ya wabia wa PPP, kanisa KKKT.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Huu ndio wakati muziki wa Singeli kutawala sanaa yetu




ENZI hizo tukiishi vijijini, maisha ya watoto waliokuwa wakiishi vijijini na wale wa mjini walitofautiana sana, huku wa mjini wakiwatambia wa vijijini kila walipokuja likizo.

Nakumbuka kuna nyakati sisi tuliofeli na kubaki vijijini kwa kukosa nafasi za kuendelea na masomo, tulionekana watu baki tusio na maana kulinganisha na waliofaulu wakaenda sekondari mjini.

Tulikubaliana na maisha hayo, kwani ndivyo tulivyopangiwa na Mungu tukaendelea kuchunga mifugo ambayo wazazi wetu waliiuza kwa ajili ya kulipia ndugu zetu wa sekondari. Tuliyazoea maisha hayo, ingawa kwa wazazi tulionekana sisi wa kazi gani, kwa sababu tofauti yetu na wale wa mjini, ilikuwa sawa na mbingu na nchi, tukionekana watumwa wa ndugu zetu wa sekondari.

Ilikuwa kawaida wakija likizo, basi tulikuwa kama watumwa wao tena tukilala chini na kuwapisha wa sekondari, ambao kwa kuwatazama tu hata mavazi yao uliweza kubaini nani wa mjini na nani wa kijijini.

Walituzuga kwa mavazi ya kigeni, wakivalia dengrizi ambazo leo tunaziita jinzi, wakivaa raba mtoni, huku sisi tukivalia kaptula tena wakati mwingine vifua wazi na chini tukiwa na makatambuga. Kwa hali hiyo, wazazi wakaweka matumaini makubwa kwa wenzetu wa sekondari, kwamba ndio watakuja kuwakomboa uzeeni, kwani walikuwa na imani kwa amalizaye sekondari lazima atapata ajira mjini.

Hivyo, wazazi wakajipangia kuwa baada ya ndugu zetu hao kumaliza masomo na kupata kazi na kuishi mjini, basi wazazi wetu nao watahamia huko kwani, kuna kila kitu na kila aina ya maisha. Tulivumilia tukifanya shughuli zetu za kawaida za kilimo na ufugaji, kidogokidogo tukabuni viwanda vidogo vya kusindika maziwa, pia mazao huko huko vijijini na kutoboa.



**NA JOSEPH KULANGWA**
**(+255) 713 410008**
**kulangwasos@gmail.com**

Ndugu zetu nao wakamaliza elimu zao, lakini tukaja kuambiwa kuwa wanarejea nyumbani kwa sababu mjini hakuna tena ajira.

Waliporejea nyumbani sisi ndio tukawa tunawabeba kutokana na miradi yetu.

Walipatikana wafadhili wakatuona na kutusaidia kukuza miradi yetu na ndipo wazee wakafumbuka macho na kutuona kama tuna msaada zaidi kuliko jamaa zetu walitarajia kupata ajira. Kumbe walipotea, ikawa zamu yetu.

Nimeikumbuka historia hii, baada ya hivi karibuni kushuhudia Serikali ya Ufaransa nchini kupitia ubalozi wake jijini Dar es Salaam, kutoa fungu la fedha kwa ajili ya kufadhili muziki wa Singeli.

Huu ni muziki ambao ulidharauliwa na baadhi ya watu na kuonekana usio na maana mbele ya Bongo*eva, Hip Hop na mingine ya kufokafoka, iliyovamiwa na vijana wetu wakiiga mirindimo ya kigeni na kudharau hata Mnanda.

Kila wasanii wa singeli walipokuwa wanachomoza pua mbele ilikatwa na Bongofleva, lakini leo wamepatikana wafadhili wanaoelewa ni nini maana ya asili ya binadamu, kwamba usiache mbachao kwa msaala upitao.

Hatua hii ilitekelezwa na kituo cha Utamaduni cha Ufaransa cha Alliance Francaise, inafanya sasa Tanzania tutambue kuwa huu ndio muziki wetu hasa utakaoitambulisha nchi hii.

Mimi nachukulia kuwa singeli ndio sisi tuliokuwa vijijini, huku kina Amapiano, Hip Hop na mingine ya kigeni ikiwa sekondari na kurudi vijijini kututambia, lakini leo watakiona cha moto baada ya mradi huu wa shilingi bilioni 1.6 kufanikiwa.

Kama alivyobainisha Balozi wa Ufaransa nchini, Nabil Hajlaoui bulungutu hilo litatumika pia kutafuta vipaji vya muzuki wa singeli katika mikoa ya Tanga, Dar es Salaam na Morogoro.

Kwa kuwa sasa muziki huu utavuka mipaka na kutangazwa ughaibuni, ni dhahiri tutasikia wazungu wakiuiga na kuupiga kama ambavyo wasanii wa Tanzania wanavyoiga muziki wa Nigeria na Afrika Kusini na kutelekeza wa kwao. Naamini hata viongozi wetu walikuwa wakidhani Amapiano na muziki wa kinaigeria ndio muziki mzuri na hata kuwapa nafasi katika matamasha na sherehe mbalimbali, sasa watakumbatia chao na kukikuza.

Lakini, wasanii ambao wanadhani bila kuimba Kiingereza hawajaimba muziki waone kuwa sasa singeli inaingia kwa namna nyingine na itajulikana na kuitangaza Tanzania kama muziki wa asili wa nchi hii.

Ni imani yetu kuwa viongozi wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo wataelekeza nguvu kwenye uasilia wetu na kuhakikisha singeli inakuwa alama ya Taifa hili na kuachana na kunakili na kuiga muziki wa kigeni na kuupa nafasi kubwa kama mateka.

Hata bila ya kutaja majina, wasanii wa Bongofleva wanaodhani kuwa muziki ni Amapiano na muziki ni wa kinaijeria, basi muda umefika wa kuwa na muziki asili ya Tanzania ambao ni Singeli.

**Alamsiki!**

UCHUMI

TARI MAKUTUPORA:

# Tumetimiza kivitendo agizo la Majaliwa, kubuni mbegu ya zabibu yenye tija kitaifa

• Kinachofuata; kuisambaza kitaifa na mageuzi katika mavuno

**Na Renatha Msungu**, DODOMA

ZABIBU hadi sasa imo katika mazao ya kimkakati kitaifa ambayo serikali inaweka jitihada kubwa, kuhakikisha wakulima wanafanya kilimo chenye tija katika zao hilo, la kibiashara, pia waweze kujiinua kiuchumi wao na familia zao.

Kutokana na hilo, serikali imekuwa ikihimiza taasisi zilizo chini ya Wizara ya Kilimo, zinazohusiana na masuala ya utafiti wa kilimo, kuhakikisha zinafanya utafiti, ili kupata mbegu bora za zao la zabibu na kuzitawanya kwa wakulima kabla ya msimu wa kilimo kuwadia.

Kutokana na hilo, Kituo cha Utafiti wa Zao la Kilimo (TARI) Makutupora, tayari kimetekeleza agizo la Waziri Mkuu la kutaka zabibu za matunda zinazouzwa na wajasiriamali wadogo na wengi nchini, zizalishwe kwa wingi katika maeneo mbalimbali kitaifa, ili ziweze kutosheleza mahitaji ya viwanda, hasa kwenye matumizi ya kawaida ya walaji.

Hadi sasa, TARI Makutupora inatajwa kufanikiwa kwenye hilo, baada ya kufanyia utafiti mbegu za zabibu za matunda, mvinyo na kuzikausha, ili kumuwezesha sasa mkulima kuvuna kwa wingi zao hilo.

Pia ni uamuzi unaoenda mbali kwa kugusa sehemu zinazostahili kulimwa zao hilo, wakulima wakifuata kanuni za kilimo wanazopewa na wataalamu wa kilimo, ili waweze kuangukia kupata matokeo chanya.

Katika maonyesho ya NaneNane ya Kanda ya Kati yaliyomalizika hivi karibuni katika viwanja vya Nzuguni, Dodoma, TARI Makutupora waliwasilisha mbegu ya zabibu aina ya matunda, mvinyo na za kukausha ambazo inazitaja zitawasaidia wakulima kupata mavuno mengi kwenye maeneo yao ya kilimo hicho.

Kwa sasa ni zao la wakazi wengi wa mkoa wa Dodoma, wakitumia sifa bora ya mahali hapo katika ustawi wa zao hilo.



Ofisa Kilimo wa TARI Makutupora, akiwa na wanafunzi katika moja ya shamba la zabibu la kituo hicho. **Picha nyingine**, zabibu ikiwa imestawi shambani. **PICHA ZOTE: RENATHA MSUNGU**



#### MRATIBU PROGRAMU ZABIBU

Saada Hussein ni Mratibu wa Programu ya Zabibu Kitaifa , anasema TARI Makutupora ni miongoni mwa vituo 17 vya utafiti na sasa kimepewa jukumu la kufanya utafiti wa zao la zabibu, ili kuwaongezea tija wakulima.

Saada anasema, tayari wameshafanyia utafiti mbegu za zabibu na sasa zinauzwa kwa wengi katika maeneo mbalimbali nchini, hivyo nao tayari wameshapata mwarobaini wa kuhakikisha wakulima wanafanya kilimo chenye tija.

Anaeleza kuwa TARI Makutupora, ndio watafiti mahsusi wa zao la zabibu, wakiwa wameshatoa teknolojia za mbegu bora kwa ajili ya kilimo cha zabibu na tayari zimeshathibitishwa na Taasisi ya Udhibiti wa Mbegu Bora Tanzania (TOSCI), kwa ajili ya kuanza kutumika na wakulima nchini.

#### AINA ZILIZOPO

Mratibu huyo anafafanua kwamba, kuna aina tatu za zabibu ambazo ni kwa ajili ya matumizi ya matunda, ambazo ni: Ya mezani; aina ya Mvinyo; pia kwa ajili ya Kukausha.

Mratibu Programu Saada, anasema inaeleweka kwamba zabibu ni zao la kimkakati, ambalo kuanzia mwaka 2021 Waziri Mkuu, alishatoa maelekezo yake kwa TARI Makutupora, kuhakikisha zabibu za mezani zinawafikia wakulima waliko.

"Nanukuu maneno ya Waziri Mkuu, 'yaani nataka nikitembea katika baadhi ya maeneo, nikutane na zabibu za mezani, ambazo ni za matunda zinalimwa hapa nchini'..."anasema Saada.

Pia, anarejea tena kauli ya Waziri Mkuu Majaliwa 'kwanini waagize zabibu kutoka nje, ilihali uwezekano wa kulima hapa nchini upo...". Hivyo, anasema jukumu la TARI Makutupora ni kuhakikisha uwapo wa zao hilo.

Kutokana na hilo, Mratibu Saada anasema wamekwishatoa mbegu za zabibu za matunda na wako katika hatua ya kuzalisha kwa wingi hiyo miche, ili wakulima wazipate katika kiwango kinachowatosha, wakapande katika mashamba yao.

"Ndani ya miaka miwili ijayo, tunatarajia zabibu zote zinazouzwa na wakulima huku barabarani, zitakuwa ni zabibu za kutoka hapa nchini," anaahidi Mratibu Saada.

> "Ndani ya miaka miwili ijayo, tunatarajia zabibu zote zinazouzwa na wakulima huku barabarani, zitakuwa ni zabibu za kutoka hapa nchini.

#### ZABIBU NA UMWAGILIAJI

Saada anasema, mkoani Dodoma akitaja katika eneo la Mpunguzi kama mfano wake kuna kiwango cha juu cha tija na anasema kwa mtu anayefanya kilimo cha umwagiliaji, ana nafasi ya kupata wastani wa zabibu tani nane hadi 15 katika kila ekari moja anayolima.

Anasema, hiyo ni tofauti kwa mkulima anayefanya kilimo cha kusubiri mvua, mavuno yao yanaweza kugota kwa wastani wa tani moja hadi tano kwa kila ekari

Mratibu Programu huyo wa zabibu, anafafanua kwamba katika ukanda wa Chamwino, Dodoma ambako kuna ukame kidogo, kwa sababu maji yake yako chini, uzalishaji wake unaweza kuwa chini kidogo na ustawi wake unaendana na umwagiliaji mkubwa.

Kutokana na hilo, anawasisitizia wakulima wenye uwezo wa kufanya kilimo cha umwagiliaji, wajikite huko, ili kuwawezesha kufikia kilimo chenye tija, kitakachowapa mavuno mengi na kuondokana na kilimo cha mazoea cha kusubiri mvua.

Anaendelea: "Maji ni muhimu sana, ndio maana tunasisitiza kwamba mkulima atumie umwagiliaji, hata serikali inatilia mkazo kwa sababu maji ni muhimu sana katika zao la zabibu."

"Maji ni muhimu sana katika kilimo cha zabibu, hivyo ndio maana tumekuwa tukisisitiza wakulima wafuate kanuni za kilimo, ambazo wanapewa na wataalamu wa kilimo, ili waweze kufanya kilimo chenye tija,"anatamka Saada.





Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum Dk. John Jingu akisikiliza maelezo kutoka kwa Msimamizi wa Makao ya kulea watoto ya Kijiji cha Matumaini Sister Euphrasia Julius alipofanya ziara katika Makao hayo yaliyopo jijini Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Matumizi mfumo kielektroniki kupunguza ucheleweshaji kesi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Serikali Mtandao (eGA) kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, imebuni Mfumo wa kielektroniki wa usimamizi wa kesi (CMIS) unaoziunganisha taasisi zote za haki jinai ili kuondokana na ucheleweshaji wa kesi kwa kuanza kutumia uliounganisha taasisi zote za haki jinai.

Miongoni mwa kazi za mfumo huo ni kupokea taarifa za majalada ya kesi kutoka vyombo chunguzi, kufuatilia mwenendo wa majalada, kutunza kumbukumbu za uamuzi.

Akizungumza kwenye uzinduzi wa mfumo huo jana jijini hapa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, alisema mfumo huo umekamilika wakati sahihi ambao Rais Samia Suluhu Hassan anaendelea na jitihada za kuimarisha utoaji wa haki kwa wananchi.

"Mfumo huu umeunganishwa na mfumo mkuu wa serikali wa kuwezesha mifumo kubadilishana taarifa (GovESB) na umeanza kubadilishana taarifa na mifumo ya baadhi ya Taasisi za Haki Jinai kama vile polisi,

Takukuru na Mahakama, hatua hii ni katika kutekeleza maelekezo ya Rais Samia kuhusu mifumo ya serikali kubadilishana taarifa," alisema.

Alibainisha kuwa hadi sasa kesi za jinai 17,411 zimesajiliwa kwenye mfumo huo na kati ya hizo 7,361 zimeshafika mwisho na kutolewa hukumu na 10,050 zipo hatua mbalimbali za uamuzi.

Alizihimiza taasisi nyingine za umma ambazo bado zina kiwango kidogo cha utekelezaji wa jitihada za serikali mtandao kuongeza matumizi ya Tehama ili kuongeza ufanisi na kuboresha utoaji huduma kwa wananchi.

Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Pauline Gekul, alisema wizara hiyo imejizatiti kuimarisha jitihada za kuhakikisha inatengeneza mifumo madhubuti ya Tehama ili kutoa huduma bora kwa wananchi.

"Haki ni suala muhimu sana na inapaswa kutolewa kwa wakati kwani haki iliyochelewa ni sawa na haki iliyonyimwa, hivyo kupitia mifumo ya Tehama tunataka kuhakikisha haki zote zinatolewa kwa wakati," alisema.

Awali, Mkurugenzi wa Mashtaka, Sylvester Mwakitalu, alisema mfumo huo utatunza kumbukumbu zote ikiwamo hati za mashtaka na hukumu na utakuwa na uwezo wa kuonesha jalada lipo kwa wakili gani na limechukua muda gani.

Alisema watahakikisha unatumika kwa ukamilifu ili kuondoa malalamiko ya wananchi.

Kadhalika, Mkurugenzi Mkuu wa eGA, Benedict Ndomba, alisema mfumo umejengwa kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa taarifa sahihi zinazohusu uendeshaji wa mashtaka na kusaidia katika uandaaji wa mipango ya ofisi na utoaji maamuzi mbalimbali pamoja na uandaaji wa taarifa zinazowasilishwa kwenye mamlaka nyingine.

# Kampuni ya simu yaboresha utoaji mikopo kwa wateja

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KATIKA kuunga mkono jitihada za serikali za kuwakwamua wananchi kiuchumi, Kampuni ya Teknolojia na Mawasiliano ya Vodacom Tanzania PLC imeboresha utoaji mikopo kwa wateja, mawakala, madereva wa vyombo vya moto, na wafanyabiashara nchini.

Aidha, imeanza kutoa mikopo ya simu janja ili kuchochea ukuaji wa matumizi ya intaneti na uchumi wa kidijitali.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni ijulikanayo kama 'Maisha ni Kujiongeza na M-Pesa' jana jijini hapa, Mkurugenzi wa M-Pesa, Epimack Mbeteni, alisema kupitia huduma zake za M-Pawa, Songesha, Wakala Songesha, Wezesha Wakala, zimeboreshwa ili kukidhi mahitaji yao kuendana na kasi ya ukuaji wa uchumi ya kidigitali nchini na duniani.

Alisema kwa miaka 15 sasa Vodacom ina watumiaji zaidi ya milioni 17 kama inavyoripotiwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

"Mikopo hii mahususi kwa wamiliki na madereva wa vyombo vya moto na hii ni chomoka pamoja na mkopo wa ada ya bima ambapo dereva ataweza kupata mkopo wa mafuta kwenye kituo chochote cha mafuta nchini chenye huduma ya lipa kwa simu lengo ni kuwawezesha kuendelea na shughuli zao kwa usalama na kuokoa muda zaidi," alisema.

Kuhusu mikopo ya simu janja, alisema

kwa malipo ya awali ya Sh. 20,000 mteja atamiliki simu janja na kulipa kidogo kidogo kwa kima cha chini cha kuanzia Sh. 900 kwa siku.

# Wizara ya Afya yajipanga kukabiliana magonjwa mlipuko

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WIZARA ya Afya imeendelea kujiimarisha katika utayari wa kukabiliana na matukio ya dharura ya afya ya jamii na magonjwa ya mlipuko kwa kutoa mafunzo elekezi kwa waratibu wa mikoa wa vituo vya uratibu matukio ya dharura (PHEOC).

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dk. Grace Magembe, alisema hayo juzi wakati akifungua mafunzo ya waratibu wa mikoa wa vituo vya uratibu matukio ya dharura za afya ya jamii, pamoja na waratibu wa ufuatiliaji wa magonjwa na matukio yenye athari za afya ya jamii.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha Watanzania wanakuwa salama na afya bora ili kufanya shughuli zao za kiuchumi na kujenga taifa kwa ujumla.

Dk. Magembe alisema kujengewa uwezo kwa wataalam hao kutasaidia kuharakisha uchakataji wa taarifa na kuchukua hatua madhubuti na za haraka za udhibiti wa matukio hayo.

Alisema kuwa mikoa 11 ya awali ya kipaumbele ni kutokana na uwezekano wa kupata dharura mbalimbali kama magonjwa ya mlipuko kutokana na jiografia na mwingiliano wa kiuchumi.

"Mikoa na halmashauri ni ngazi muhimu katika kuleta mabadiliko (game changer) kwenye udhibiti wa matukio ya dharura ya afya ya jamii ikiwemo magonjwa ya milipuko," alisema Dk. Magembe.

Kadhalika, alisema mafunzo hayo ni sehemu ya mikakati ya kukabiliana na magonjwa ya dharura ikiwamo magonjwa ya mlipuko na ajali mbalimbali.

"Mafunzo haya yamejumuisha waratibu kutoka mikoa 11 kutoka Tanzania bara na visiwani chini ya ufadhili wa kituo cha kukinga na kudhibiti magonjwa cha Afrika (Africa CDC), Marekani (US CDC) na Shirika la Afya Duniani," alisema.

Vile vile, Dk. Magembe alisema mafunzo hayo ni sehemu ya mikakati iliyowekwa na serikali ili kuhakikisha wanailinda nchi na majanga, maafa ikiwemo magojwa ya mlipuko na ajali.

Pia, alisema hivi karibuni Tanzania ilifanyiwa tathmini na Dunia kuona utayari wa kukabiliana na dharura za magonjwa ya mlipuko, maafa na majanga.

"Kwa tathmini iliyofanyika mwaka 2006 Tanzania ilikuwa na asilimia 48 na kwa sasa matokeo ya awali tuna asilimia 63 za utayari wa kukabiliana na dharura za magonjwa ya mlipuko, maafa na majanga," alisema Dk. Magembe.



HABARI MBEYA

# Wenye ulemavu waitwa mafunzo uanagenzi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imewataka vijana wenye ulemavu kuchangamkia fursa ya mafunzo ya uanagenzi yaliyoandaliwa kwa ajili ya kuwapatia ujuzi utakaowawezesha kujiajiri katika shughuli mbalimbali za uzalishaji mali.

Taarifa ya serikali iliyotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu, inabainisha kuwa awamu ya sita ya mafunzo hayo inatarajiwa kuanza mwezi oktoba mwaka huu. Zaidi ya vijana 450 watapatiwa ujuzi wa aina mbalimbali bila malipo.

Programu ya uanagenzi inalenga kurasimisha ujuzi na stadi za kazi stahiki ili kuwawezesha vijana hao kumudu ushindani katika soko la ajira, serikali ikiingia makubaliano na vyuo 28 nchini kwa ajili ya kutoa mafunzo hayo.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, juzi alizuru katika Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) kwa lengo la kukagua mafunzo mbalimbali yanayoendelea.

Alisema aliridhishwa na hatua iliyofikiwa katika mafunzo hayo ikiwamo kuwapo vijana wenye ulemavu ambao ni miongoni mwa makundi ambayo yamekuwa hayapewi kipaombele katika shughuli za ufundi.

Aliwataka vijana wengine ambao wanatamani kupata mafunzo hayo kujitokeza ili wajiunge na awamu ya sita ambayo inaanza mwezi Oktoba. "Mafunzo haya yanayoendelea kutolewa kwa sasa ni ya awamu ya tano tangu kuanza kwa mpango huu. Katika awamu hii tulichukua vijana 3,765 na hapa nimeona wenye ulemavu hawajaachwa nyuma.

"Niwajulishe kuwa kuna tangazo la kuanza kwa mafunzo mengine niwatake vijana wenye ulemavu wajitokeze kuomba," alisema Prof. Ndalichako.

Waziri huyo pia aliwataka vijana watakapohitimu mafunzo hayo kuwa waaminifu kwenye kazi zao kwa kuepuka vitendo vya wizi na kuwa wazalendo kwa kuunga mkono jitihada za serikali na kuepukana na vitendo vinavyoweza kuleta uvunjifu wa amani.

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo cha MUST Taaluma, Prof. Godliving Mtui, alisema katika awamu ya tano ya mafunzo hayo, chuo hicho kilipokea vijana 400 ambao wanaendelea kupata ujuzi katika fani 14. Chuo kinatoa mafunzo kwa vitendo kwa asilimia 75 na nadharia asilimia 25.

Alizitaja fani zinazotolewa ni pamoja na Tehama, ufundi magari, umeme, ufundi bomba, ubunifu wa mitindo na ushonaji nguo, uchomeleaji, uashi na huduma za hoteli na utalii. Prof. Mtui alipongeza serikali kwa kubuni na kuwezesha mpango huo kwa vijana ambao utawasaidia kuajiriwa, kujiajiri na kuajiri wengine.

"Kipindi hiki ambacho ajira ni ngumu, ni vizuri sana kuwapatia vijana ujuzi ambao utawasaidia kujiajiri, sasa mafunzo hay ani muhimu sana kwa taifa letu, vijana wanapata ujuzi mzuri sana ambao unaendana na mahitaji ya soko la ajira," alisema Prof. Mtui.

Baadhi ya wanafunzi wanaoendelea kupata mafunzo hayo waliishukuru serikali kuwezesha mafunzo kupitia mpango huo.

Walisema umewawezesha kupata ujuzi mbalimbali utakaowasaidia kujiajiri huku wakiomba serikali kuwapa mikopo baada ya kuhitimu ili wapate mitaji.

Mmoja wa vijana hao, Anastazia Misabala, alisema katika kipindi ambacho amekaa chuoni hako, amepata mafunzo ambayo yatamwezesha kujiajiri.

Alisema amepata ujuzi wa kutumia Tehama na hivyo anakusudia kufungua ofisi kwa ajili ya ujenzi matengenezo ya kompyuta na kutengeneza matangazo mbalimbali. Kwa mujibu wa takwimu za serikali, tangu kuanza kwa mpango huo, jumla ya vijana 133,448 wamenufaika kwa kupata mafunzo hayo katika vyuo vilivyoteuliwa.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makudi Maalumu, Dk Dorothy Gwajima akisoma na kufuatilia hotuba ya Mbunge wa viti maalumu Mkoa wa Tanga Mwanaisha Ulenge jana kabla ya kufunga kongamano la Wanawake na Manunuzi ya Umma, Fursa za Biashara katika Bomba la Mafuta, Ulenge pia ni Mkurugenzi wa Taasisi ya Daraja Foundation, wa pili ni Waziri wa Afya Ummy Mwalimu, ambaye ni mbunge wa Tanga. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

## TANESCO yanyooshewa kidole kukwaza ibada

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UONGOZI wa Mkoa wa Mbeya umeliagiza Shirika la Umeme (TANESCO) kutokata umeme siku za Ijumaa, Jumamosi na Jumapili ili kuwasaidia waumini wa madhehebu mbalimbali kusali.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alitoa agizo hilo juzi wakati wa kikao maalum na viongozi wa dini mkoani mwake, akisisitiza nishati hiyo ni muhimu kwa waumini.

Homera alitoa agizo hilo baada ya viongozi wa dini kulalamikia kukatika nishati hiyo na kuwafanya walazimike kutumia gharama kubwa kupata nishati mbadala

"Hata kama kuna marekebisho wanayafanya, basi angalau waache siku za ibada ambazo ni Ijumaa, Jumamosi na Jumapili, watu wasali na watumie vyombo vyao vizuri," alisema Homera.

Baadhi ya viongozi wa dini walisema umeme unapokatwa siku za ibada, wanalazimika kutumia jenereta na hivyo kutumia gharama kubwa kununua mafuta.

Mmoja wa viongozi hao wa dini, Thomas Kongoro, alisema wakati wa ibada umeme unapokatika huwa wanashindwa kuendesha vizuri ibada.

Aliomba serikali kuwasaidia ili kupunguza gharama za kuendesha ibada, akieleza kuwa huwa wanalazimika kununua petroli.

# Sababu tatu za ugonjwa wa TB kusumbua Njombe

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WATU 252 wamefanyiwa vipimo vya ugonjwa wa kifua kikuu (TB) huku 30 kutoka Kata ya Luponde na sita kutoka mjini Njombe wakigundulika kuwa na ugonjwa huo na kuanzishiwa matibabu.

Mratibu wa Kifua Kikuu na Ukoma Halmashauri ya Mji Njombe, Dk. Mashaka Kisulila, alibainisha hayo juzi alipotoa tathmini ya kliniki tembezi iliyolenga kufanya upimaji kwa ugonjwa wa TB na Ukimwi.

Dk. Kisulila alitaja sababu kuu tatu zilizo miongoni mwa vihatarishi vinavyochangia kuwapo kwa ugonjwa wa TB mkoani Njombe ni uhusiano wa moja kwa moja wa TB na Virusi vya Ukimwi (VVU), lishe duni na hali ya hewa ya baridi kali.

"Maambukizi ya VVU Njombe bado yapo kwa kiasi, lakini pia watu wengi hawapati lishe bora, hivyo kusababisha kinga ya mwili kuwa chini, jambo ambalo ni hatari kwa kuwa mwili unakuwa hauwezi kukabiliana na mashambulizi ya virusi. "Jambo lingine, Njombe kuna baridi kali na ujenzi wa nyumba wengi hupenda kuziba ili kuweka joto ndani, jambo ambalo linasababisha mzunguko wa hewa safi ndani kuwa mdogo na kuweka hatari kwa TB," alisema Dk. Kisulila.

Alieleza mikakati waliyonayo kuhakikisha wanazuia na kutokomeza TB, zikijumuisha kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kupitia vyombo vya habari na kusisitiza wananchi kuwahi matibabu, kuzingatia ushauri na matumizi sahihi ya dawa ambayo hutolewa bure katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya.

"Niombe jamii kujenga utamaduni wa kupima afya mara kwa mara ili kutambua hali zao za afya na kupunguza athari zitokanazo na magonjwa sugu," alisema Dk. Kisulila.

Baadhi wa wananchi mjini Njombe, waliwashukuru wataalamu wa afya, wakishauri kuwe na jitihada zaidi kuelimisha jamii ili iwe na utamaduni wa kupima afya zao na kutokusubiri madhara.

"Hii tabia ya kusubiri hadi tutembelewe sio nzuri kwa sababu ukipima na kujua hali yako, itakufanya uwe huru na upate ushauri wa wakati sahihi," alisema Actovian Sanga. Naye Janet Lwiva alisema: "Mimi ninaona tunatakiwa kubadilika, muda mwingi tunatumia kwenye kazi na kusahau afya zetu ambazo zikiteteleka, hata hizo kazi hatuwezi kufanya."

Wizara ya Afya kwa kushirikiana na ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Njombe imefanya kliniki tembezi bila malipo kwa ajili ya kupima na kugawa kinga tiba dhidi ya TB mjini Njombe.





# Wawekezaji China kuwekeza kilimo cha muhogo, maharage

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KUFUATIA ziara ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi nchini China hivi karibuni, ujumbe wa wawekezaji kutoka nchini humo umefika visiwani Zanzibar kwa ajili ya kuwekeza Tanzania katika miradi mbalimbali ikiwamo kilimo cha muhogo na maharage na kuanzisha kiwanda cha utengenezaji wa pikipiki. Akizungumza jana katika kikao cha majadaliano kati ya wawekezaji hao na watendaji wa serikali ikiwamo Mamlaka ya Uwekezaji na Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA), Mkurugenzi wa ZIPA, Sharifu Ali Sharifu, alisema wawekezaji hao wameitikia wito kuja nchini kutafuta fursa. Alisema wamepokea maombi ya kampuni kutoka China kwa ajili ya kuwekeza miradi ya viwanda vya kuzalisha na kuunganisha pikipiki.

"Tumepokea maombi ya wawekezaji kutoka China kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda vitakavyozalisha pikipiki za aina mbalimbali ikiwamo za mafuta na umeme," alisema.

Alisema miongoni mwa maeneo waliyolenga kuwekeza ni kilimo hasa katika zao la muhogo ambalo kufuatia mpango huo litaingia kwenye sehemu ya zao la mkakati na China linahitajika kwa kiwango kikubwa.

Sharif aliwataka vijana kuchangamkia fursa za ajira kupitia wawekezaji wanaoendelea kuwekeza nchini na kuwa tayari kwa kujitayarisha ikiwamo kuwa na elimu za fani muhimu zinazoweza kuwaletea maslahi.

Mwakilishi wa jumuiya ya wafanyabiashara na wakulima wa diaspora kutoka China, John Rwehumbiza, aliwataka wakulima kuchangamkia fursa za kilimo cha mazao ya muhogo, ufuta pamoja na maharage ya soya ambayo soko na mahitaji yake nchini China ni kubwa na linaweza kuleta mageuzi makubwa ya kukuza uchumi wa wakulima.

"China inaongoza duniani kwa mahitaji ya zao la muhogo ambapo teknolojia imeongezeka katika ununuzi wa muhogo mbichi, hivyo wakulima changamkieni fursa hiyo," alisema.

Aidha, alisema fursa nyingine kwa wakulima wa Tanzania ni kilimo cha ufuta pamoja na maharage aina ya soya ambapo mahitaji yapo zaidi ya tani milioni mbili.

Alisema kampuni za China zipo tayari kutoa elimu na utaalamu ambao utawawezesha wakulima wa Tanzania kulima kwa kutumia mbinu za kisasa za kitaalamu ambazo zitawawezesha kuvuna na kupata kipato kikubwa.

"Wenzetu wa Thailand wanalima ekari moja ya maharage aina ya soya na kuvuna tani 20 wakati sisi ekari moja tunavuna tani moja," alisema.

Rwehumbiza alisema wawekezaji kutoka China wakiwa na ujumbe wa kampuni 15 wapo nchini wakiwa tayari kuwekeza katika sekta ya viwanda kwa kuanzia kujenga viwanda viwili vya kuzalisha pikipiki zinazotumia mafuta kwa gharama nafuu na umeme.

"Tupo na ujumbe wa wawekezaji wa kampuni 15 kutoka China ikiwa ni matokeo ya ziara ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliyoifanya China tukiangalia fursa za uwekezaji Zanzibar," alisema.

Naye kiongozi wa ujumbe huo kutoka China, William Chu, alisema wapo tayari kuwekeza Zanzibar na wameridhishwa na mazingira ikiwamo utulivu wa kisiasa na jiografia yake.



Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar Othman Masoud Othman, akimsikiliza Rais wa shirika la Kimataifa linalojishughulisha na kuwezesha maendeleo endelevu kwa jamii (PACT) Dk. Caroline Anstey, lenye makao makuu yake nchini Marekani. Ujumbe huo ulifika ofisini kwa Makamu Migombani mjini Zanzibar jana kwa kubadilishana mawazo na Makamu huyo wa Rais. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS**

# Kiwanda kuchakata mwani mbioni kukamilika

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Zanzibar imesema ipo katika hatua ya kukamilisha ujenzi wa kiwanda cha kuchakata mwani kilichopo Chamanangwe, Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Imesema kukamilika kwa kiwanda hicho ni suluhisho la kilio cha wakulima wa mwani Zanzibar na kuongeza thamani ya zao hilo.

Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, aliyasema hayo wakati akizungumza na wanachama wa CCM na wananchi wa Jimbo la Pandani na Kojani akiwa katika muendelezo wa ziara yake ya kuimarisha chama Mkoa wa Kaskazini, Pemba.

Alisema katika kutekeleza Ilani ya CCM, serikali ipo katika hatua za mwisho kukamilisha ujenzi wa kiwanda hicho ambacho kitawanufaisha wakulima wa mwani na kitatoa fursa nyingi za ajira kwa wananchi.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itahakikisha zao la mwani linauzwa kwa bei ya juu na kuwataka wananchi wa kisiwani Pemba waitumie vyema fursa hiyo ili kujikwamua na ukali wa maisha.

Aidha, alisema serikali kupitia mfuko wa uwezeshaji wananchi kiuchumi itawawezeshwa wakulima wa zao la mwani vifaa vyote vya kulimia ikiwamo Kamba na Taitai ili kulima bila ya kikwazo chochote.

Alisema anatambua kuwa Mkoa wa Kaskazini Pemba ni maarufu kwa shughuli za uvuvi na serikali imejipanga kuwaimarisha kupitia sekta ya uchumi wa buluu kwa kuwapatia boti za kisasa zenye mashine na mitego yenye uwezo mkubwa wa kuvua bahari kuu ili kupata mazao mengi na yenye tija kwa taifa.

Mjumbe wa Kamati ya Siasa Wilaya ya Wete, Hamad Omar Bakari, alisema miundombinu ya mabomba ya maji wilayani humo ni chakavu na serikali inaandaa mradi wa maji uitwao Zanzibar Water Security Project (ZWSP), ambao upo hatua za awali kuanza na utamaliza tatizo la hilo Pandani na maeneo jirani.

Alisema Wizara ya Afya inasimamia ahadi ya Rais Dk. Mwinyi kuwajengea kituo cha afya Kiungoni ambacho tayari mipango ya awali imeshaanza ili kumaliza changamoto inayowakabili wananchi wa eneo hilo kufuata huduma hiyo masafa marefu.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa kupitia Jumuiya ya Wazazi, Habiba Ali Muhamed, aliwataka vijana kutumia fursa ya elimu bila ya malipo inayotolewa na serikali ili kupata elimu bora yenye manufaa kwao.

# Othman ataka suluhisho tatizo la ajira kwa vijana

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema suala la ukosefu wa ajira kwa vijana wa Zanzibar linaendelea kuwa changamoto kubwa inayohitaji jitihada za pamoja kwa ushirikiano kati serikali na wadau mbalimbali wa maendeleo katika kuandaa sera na mipango sahihi na kuweka mikakati madhubuti ya utekelezaji katika kulikabili kwa ufanisi suala hilo.

Othman aliyasema hayo ofisini kwake Migombani mjini hapa alipofanya mazungunzo na Shirika la Kimataifa lisilo la Serikali (PACT), ambalo kwa kushirikiana na serikali mbalimbali duniani linajishughulisha kuwezesha maendeleo endelevu kwa jamii, uimarishaji wa utawala bora na Demokrasia, na kuhudumia watu wenye changamoto na kuleta afua katika sekta za lishe, elimu, uwezeshaji kiuchumi na utafutaji wa masoko.

Alisema tatizo hilo ni kubwa na limekuwa likiongezeka kwa kasi kila mwaka kwa kuwa vijana wengi wanaendelea kukosa ajira na hivyo kuashiria kwamba jambao hilo linaweza kugeuka kuwa ni janga la baadae katika nchi jambo ambalo linahitaji jitihada kubwa katika kuwawezesha vijana kwa kutumia rasilimali za ndani zilizopo hasa katika sekta ya utalii.

Kadhalika, alisema Zanzibar hivi sasa ina hoteli za utalii zaidi 600, lakini mahitaji makubwa ya hoteli hizo yanapatikana kutoka nje ya Zanzibar, na iwapo vijana nchini watawezeshwa ipasavyo sekta hiyo pekee inaweza kuwa na uwezo na kutoa fursa kubwa za kutatua tatizo la ajira kwa vijana nchini.

Kupitia juhudi za pamoja kati ya serikali na taasisi zisizo za serikali kama vile PACT, alisema inawezekana kuwawezesha vijana kujengewa uwezo wa kujiajiri katika uzalishaji wa bidhaa mbalimbali zinazohitajika katika soko la utalii jambo ambalo litasaidia sana katika kuikabili changamoto ya ukosefu wa ajira nchini.

Alisema, serikali haina uwezo wa kuwaajiri vijana wote waliopo na wanaomaliza katika vyuo vikuu, lakini kinachohitajika ni kuwapo mazingira sahihi ya kuwawezesha katika sekta ya biashara ya utalii na ukarimu na kwamba bila kuwawezesha vijana katika ajira taifa haliwezi kuwa na mabadiliko chanya kimaendeleo.

Vijana katika taifa lolote, alisema wanapaswa kuandaliwa kuwa chachu ya mabadiliko ya kimaendeleo kwa kuangalia mahitaji yao muhimu kwa sekta na maeneo tofauti kwa kuzingatia mahitaji ya wakati wa sasa na wa baadaye ili taifa liweze kupiga hatua zaidi na kwa haraka.

Akizungumzia suala la athari zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi, alisema Zanzibar kuna maeneo yapatayo 14, yamekumbwa na athari hiyo ingawa juhudi kubwa zimekuwa zikichukuliwa na serikali ikiwa ni pamoja na upandaji wa mikoko lakini tatizo la athari hizo bado linaendelea katika maeneo mbali mbali nchini.

Hata hivyo, alisema serikali inaendelea na mikakati mbalimbali ya kitaifa na hivi karibuni itazindua mradi wa kuirejesha Zanzibar kuwa ya kijani utekelezaji wake utahitaji ushiriki wa wadau wa maendeleo katika kufikia ufanisi wa lengo lililokusudiwa la kupunguza athari za mabadiliko ya tabia nchi.

Akizungungunzia suala la vijana katika siasa Othman, alisema kwamba wengi wao wanaingia kwa matumaini ya kupata ajira badala ya kufikiria kuwapo mabadiliko ya kimaendeleo jambo ambalo linabakia kuwa ni changamoto kwa kwa vijana.

Naye Rais wa PACT, Dk. Caroline Anstey, alisema shirika hilo limekuwa likifanya kazi kubwa na jamii katika nchi mbalimbali duniani katika kuweka ustawi wa masuala ya afya kwa jamii pamoja na kusaidia kujenga uwelewa kwa vijana katika masuala ikiwemo demokrasia, elimu na utawala bora.

Alisema kwamba shirika hilo lenye makao yake makuu nchini Marekani lipo tayari kufanya kazi na serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika maeneo mbalimbali ya kuwawezesha vijana katika masuala ya elimu, afya, ustawi wa jamii na demokrasia pamoja na utawala bora na hivi sasa wanafanya kazi katika

nch

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI NA RESULT SLIP



**OSAKWE AMOUR SALEH** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita na result slip ya kidato cha sita vyenye index namba **S1197/0629** vilivyotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **GREEN ACRES SECONDARY SCHOOL** mwaka 2007. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/3036/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MAMA SAVANA SAFARI'S COMPANY LIMITED** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA LANDCRUISER** yenye usajili namba: **T 461 ASH ,** CHASSIS NAMBA: **JTELB71J207065376** na ENGINE NAMBA: **IHZ0548967.** Kwa yeyote atakaiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA: **PHQ/ARU/ARU/692/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MARTHA STEPHEN LUKUMAY** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye jina **NAM ENTERPRISES LTD.** namba za usajili **T 217 AMJ** aina ya **TOYOTA TERCEL,** Chassis No. **EL530193557,** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu.

Taarifa ya polisi; **PHQ/DOD/DOD/891/2023**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA DISTRICT AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.78 OF 2023**

**In the matter of the Estate of the late MAGENI YACOB CHANDIKA of Dodoma city**

**AND**

**In the matter of an application for letters of administration by HELLENA STEPHEN MPUYA**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of administration is made to the above named Petitioners.

Objections to the grant should be filed on or before the 14 Day of 9, 2023.

**Dated at Dodoma this 24 day of 8, 2023.**

RESIDENT MAGISTRATE

NYADHI INVESTMENT Co. LIMITED
T/A
NYADHI INVESTMENT Co. LIMITED AUCTION MART

**SHAURI NA. 108/2023**
**31/07/2023**
**YUSUPH MANASE – MDAIWA**
**S.L.P**
**TANZANIA**
**____________________**
**SAHIHI YA MDAIWA (NATHIBITISHA KUPOKEA)**

**YAH : ILANI YA KUKUTAKA KUMLIPA INSP NYAMWAILA KIASI CHA SHILINGI ZA KITANZANIA MILIONI KUMI (10,000,000/=)**

KWA AMRI NILIYOPEWA NA MAHAKAMA YA MWANZO KISESA, NAKUAMURU KUMLIPA INSP NYAMWAILA KIASI CHA SHILINGI ZA KITANZANIA 10,000,000/=. PAMOJA NA GHARAMA ZETU ZA UTEKELEZAJI WA AMRI HII, KIASI CHA SHILINGI ZA KITANZANIA 740,000/= AMBAZO JUMLA YAKE NI SHILINGI ZA KITANZANIA 10,740,000/=. GHARAMA ZINAWEZA KUONGEZEKA ENDAPO UTAKAIDI KULIPA DENI HILI MPAKA KUFIKIA KUKAMATWA/KUUZWA KWA MALI ZAKO.

UNATAKIWA KUFANYA MALIPO NDANI YA SIKU 14 TU ZA KAZI, KUANZIA LEO TAREHE 25/08/2023 HADI TAREHE 15/09/2023. NA BAADA YA MUDA HUO KUISHA BILA KUFANYA MALIPO HAYO, BASI HAKUTAKUWA NA TAARIFA NYINGINE ZAIDI NI KUKUCHUKULIA HATUA KALI ZA KISHERIA IKIWA NI PAMOJA NA KUKAMATWA/KUUZA MALI YAKO/ZAKO KWA AMRI YA MAHAKAMA.

Wako,
Noemia Samwel Nyadhi,
Dalali Wa Mahakama

## OFISI ZA MATANGAZO

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0745 700 710.

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

# Nani anahusika kifo cha Prigozhin?



Mabaki ya ndege inayoaminika alikuwamo Mkuu wa Kundi la Wagner, Yevgeny Prigozhin. **PICHA:REUTERS**

**MOSCOW,** Russia

DUNIA imepigwa na butwaa baada ya kiongozi wa kundi la wanamgambo wa Wagner nchini Russia, Yevgeny Prigozhin kufariki dunia katika ajali ya ndege

Mamlaka ya Russia imesema kiongozi huyo ni miongoni mwa watu 10 waliofariki baada ya ndege waliyokuwa wakisafiria kuanguka na kuteketea kwa moto hapo juzi jioni.

Ukurasa wa mtandao wa Telegram wenye jina la Grey Zone, ambao una mafungamano na Kundi la Mamluki la Wagner, uliripoti kuwa Prigozhin amekufa katika ajali hiyo.

Ujumbe kwenye ukurasa huo ulimtaja kama shujaa na mzalendo ambaye amepoteza maisha kwa mikono ya watu wasiojulikana na kuwataja kuwa wasaliti wa Russia.

Mamlaka za Russia zilichapisha orodha ya watu waliopoteza maisha katika ajali ya ndege iliyotokea jana jioni likiwemo jina la Yevgeny Prigozhin.

Orodha hiyo ilitolewa na Wakala wa Usafiri wa Anga nchini humo, na kujumuisha majina ya watu 10 ambayo mbali ya Prigozhin limo la mtu wake wa karibu Dmitry Utkin, ambaye alimsaidia kuliunda kundi la Wagner.

Ndege hiyo ilikuwa ikisafiri kutoka mji mkuu wa Moscow kwenda kuelekea mji wa St Petersburg.

Hata hivyo, ilianguka karibu na kijiji cha Kuzhenkino kilichopo kwenye mkoa wa Tver, kulingana na Wizara ya Huduma za Dharura nchini Russia.

Wapelelezi nchini humo walisema wamefungua uchunguzi wa jinai kubaini sababu ya kuanguka kwa ndege hiyo ya binafsi iliyombeba Prigozhin.

Baadhi ya vyanzo ambavyo havikutajwa majina vimeviambia vyombo vya habari vya Russia kwamba vinaamini ndege hiyo iliangushwa na kombora la mifumo ya ulinzi.

Hakuna taarifa yoyote iliyotolewa na Ikulu ya Russia ya Kremlin, wala Wizara ya Ulinzi ya nchi hiyo kuhusiana na kifo cha Prigozhin.

Kiongozi wa kundi la Wagner alionekana adui wa watawala wa jeshi la Russia, kutokana yeye mwenyewe kuwatuhumu kwa uwezo mdogo wa kuendesha vita vya nchini Ukraine.

Wafuasi wake wameinyooshea kidole serikali ya Russia kwa kifo hicho na wengine wameitupia lawama Ukraine kuwa nyuma ya tukio hilo.



Kiongozi wa Wagner, Yevgeny Prigozhin.

Katika jengo la ofisi za kundi la Wagner mjini St Petersburg, taa ziliwashwa wa katika umbo lenye kuonyesha alama ya msalaba ambayo imetafsiriwa na wengi kuwa ishara ya kuomboleza na kutoa heshima kwa Prigozhin.

### MWANZO WA HOFU

Prigozhin mwenye umri wa miaka 62 aligonga vichwa vya habari duniani baada ya kuongoza uasi uliodumu kwa muda mfupi dhidi ya mamlaka za Russia Juni 23 hadi 24 mwaka huu.

Wapiganaji wa Wagner walizidungua helkopta za kijeshi na kuwauwa marubani na huku wakisonga mbele kuelekea mji mkuu Moscow.

Jeshi la Russia lilighadhabishwa na kitendo hicho ambacho Rais Vladimir Putin alikiita sawa na usaliti uliotishia kutumbukiza nchi hiyo katika vita ya wenyewe kwa wenyewe.

Prigozhin alifanya uasi huo baada ya miezi kadhaa ya kulikosoa waziwazi Jeshi la Russia kwa jinsi linavyoendesha vita nchini Ukraine na alijaribu mara kadhaa kushinikiza Waziri wa Ulinzi wa nchi hiyo Sergei Shoigu na Mkuu wa Majeshi waondolewa madarakani.

Uasi huo wa Wagner ulisitishwa kufuatia makubaliano yaliyofikiwa kwa Prigozhin kuridhia kwenda Belarus.

Hata hivyo alikuwa na ruhusa ya kufanya safari bila kizuizi ndani ya Russia.

### SERIKALI YAHUSIKA?

Tangu kusambaa taarifa za ajali hiyo, maoni kutoka kwa viongozi mbalimbali a kimataifa yalimiminika.

Rais Joe Biden wa Marekani alipoulizwa na waandishi wa habari kuhusu mkasa huo, alijibu hana taarifa za kutosha lakini hakuna kilichomshangaza akisema karibu kila kinachotokea nchini Russia kuna mkono wa Rais Vladimir Putin.

Abbas Gallyamov, mwandishi wa zamani wa hotuba za Rais Putin ambaye sasa ni mkosoaji wa utawala wake, alisema kiongozi huyo anahusika na ajali hiyo ya ndege.

Alisema kilichotokea kimeimarisha nafasi yake ya mamlaka kuelekea uchaguzi wa mwaka ujao ambao Putin anatarajiwa kuwania muhula mwingine.

Mkosoaji mwingine na mfanyabiashara maarufu kutoka Russia, Bill Browder, anakubaliana na mtizamo wa kuwa Putin anahusika kwenye ajali hiyo iliyomuua kiongozi wa kundi la Wagner.

"Putin kamwe huwa hasamehi wala kusahau na kitendo cha uasi kilichofanywa na mkuu wa kundi la Wagner kilimfedhehesha na isingekuwa rahisi akubali kumwacha Prigozhin akitamba duniani bila kuchukuliwa hatua" alisema.

### MIILI YAPATIKANA

Huduma za dharura za Russia zilisema kuwa miili ya abiria wote kumi kwenye ndege hiyo ya Embraer Legacy imepatikana.

Kulingana na mamlaka hiyo, waliokuwemo ndani ya ndege hiyo ni pamoja na bosi wa Wagner Yevgeny Prigozhin na kamanda wake wa pili Dmitry Utkin.

Juhudi sasa zinaelekezwa kubaini juu ya kile kilichosababisha ajali hiyo.

Polisi waliziba eneo lote karibu na sehemu iliyoangukia ndege na Mamlaka ya Usafiri wa Anga ya Russia imeunda tume maalum kuchunguza ajali hiyo.

# Mabalozi wapigwa msasa kuhusu uwekezaji

**Na Joseph Mwendapole**

KITUO cha Uwekezaji Tanzania (TIC), kimeanza kuwanoa mabalozi kuhusu fursa mbalimbali za uwekezaji zilizoko nchini ili kuhamasisha wawekezaji wa kigeni wanapokwenda kuiwakilisha Tanzania.

Mabalozi hao ni wale walioteuliwa na kuapishwa hivi karibuni na Rais Samia Suluhu Hassan ambaye wakati akiwaapisha aliagiza wapewe mafunzo ya aina hiyo.

Waliopata mafunzo hayo jana ni pamoja na Balozi Mteule wa Canada, Joseph Sokoine, Balozi wa Oman Fatma Rajabu, Naimi Aziz wa Austria na Ali Mwadini ambaye anakwenda Ufaransa.

Akizungumza baada ya mafunzo hayo jana, Mkurugenzi wa Uhamasishaji Uwekezaji wa TIC, John Mnali, alisema mafunzo hayo yatakuwa endelevu kwa mabalozi wote wanaoiwakilisha Tanzania kwenye mataifa mbalimbali.

"Kama mnavyokumbuka Mheshimiwa Rais wakati akiwaapisha mabalozi hawa wapya alisema wapewe mafunzo ya uwekezaji. Kwa hiyo tumeanza kutekeleza maagizo hayo na mafunzo yatakuwa endelevu kwa mabalozi wote," alisema.

TIC, alisema imewaeleza mabalozi hao maboresho mbalimbali ambayo wamefanya katika kuvutia uwekezaji kwa wawekezaji wote wanaokuja kuwekeza nchini. Mnali alisema, wamewapatia vitendea kazi mbalimbali ambavyo mabalozi hao watavitumia kuvutia na kuhamasisha uwekezaji watakapokuwa kwenye mataifa hayo wakiiwakilisha Tanzania.

Alisema wamewaambia mabalozi hao kuhusu umuhimu wa kutafuta fursa za uwekezaji kwenye ujenzi wa viwanda ambavyo vitatengeneza bidhaa mbalimbali ambazo malighafi zake zinapatikana nchini.

"Hili tunalisisitiza kwa sababu uwekezaji wa aina hii utasaidia kuleta manufaa makubwa sana Tanzania kwa sababu kama malighafi zitatoka hapa nchini ina maana hata nafasi za ajira zitaongezeka na wananchi wengi watapata kipato cha uhakika kwa kupeleka malighafi kwenye viwanda vya aina hiyo," alisema Mnali.

Alisema miongoni mwa mambo mazuri ambayo yamefanywa na TIC ni maboresho ya Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 2022. Kutokana na maboresho hayo, alisema kiwango cha uwekezaji kwa Mtanzania mzawa kimeshuka hadi Dola za Marekani 50,000.

"Miradi ya upanuzi kwa mwekezaji yoyote ambaye ameshaka nchini na kuwekeza, kupitia mabadiliko ya sheria hii atapata vivutio vya uwekezaji.

"Hata kwenye miradi ya ukarabati kwa mfano mwekezaji anamradi ambao haukuweza kufanya vizuri sana akitaka kufanya ukarabati sheria inampa vivutio vingi tofauti na mwekezaji mpya," alisema

Mnali alisema jambo lingine zuri kwenye mabadiliko ya sheria ya mwaka 2022 ni kwamba muda wa kuhudumia uwekezaji nchini umepunguzwa kutoka siku 14 hadi saba.

"Kwa sheria ya zamani mwekezaji anapoomba leseni au kibali maalum, sheria ilitaka ahudumiwe ndani ya siku 14 lakini kwa mabadiliko yaliyofanyika atahudumiwa ndani ya siku saba. Sheria inataka awe amepata majibu ya vibali vyake na leseni alivyoomba kupitia TIC," alisema Mnali.

Balozi Sokoine aliishukuru serikali kwa uamuzi wa kuwapa mafunzo hayo na aliahidi kuyatumia kuhamasisha uwekezaji mpya wa sekta mbalimbali kutoka Canada.

"Kwa uhakika mafunzo haya yametufumbua macho kuhusu fursa nyingi za uwekezaji zilizoko nchini na sisi wawakilishi tutawaambia wawekezaji waje kuwekeza kwenye sekta ya kilimo, madini, viwanda kuongeza thamani ya mazao tunayozalisha ili tuuze nje bidhaa na kuingiza fedha za kigeni na kuongeza ajira," alisema.

Naye Balozi Rajabu alisema moja ya vipaumbele vya serikali ni kutangaza diplomasia ya uchumi kwa hiyo watatumia mafunzo hayo kutangaza uwekezaji na vivutio vya utalii.

"Tumenufaika sana na mafunzo haya na TIC wamefanya maboresho makubwa sana ya kuifanya iwe na huduma za mahala pamoja na wamefanya maboresho makubwa ya sheria ambayo yatasaidia kutangaza fursa na tutapata wawekezaji wapya wengi," alisema.

# JOB AWEKA REKODI MPYA YANGA UFUNGUZI LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

USHINDI wa mabao 5-0 iliyoupata Yanga katika mechi yake ya kwanza ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam juzi imeifanya kuwa wababe dhidi ya KMC mara nane katika michezo 11 waliyokutana.

**Pia beki wake, Dickson Job ameweka rekodi ya kuwa mchezaji wa kwanza kufunga bao la msimu huu katika kikosi hicho.**

Hakuna beki yoyote wa Yanga aliyefunga bao la kwanza la timu hiyo kwa zaidi ya misimu 16.

Yanga pia inashinda mechi ya kwanza ya Ligi Kuu Bara kwa misimu miwili mfululizo, huku ikipata ushindi wa idadi kubwa ya mabao katika mchezo wa ufunguzi mara ya kwanza baada ya misimu tisa.

Kwa mujibu wa rekodi zilizopo ni msimu uliopita ilianza ligi kwa ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Polisi Tanzania, lakini msimu wa 2020/21 ilianza kwa sare ya goli 1-1 dhidi ya Prisons, mabao yaliyofungwa na Michael Sarpong huku Lambart Sabianka akiwafungia Wajelajela.

Mara ya mwisho Yanga kushinda mabao mengi katika mechi ya kwanza ya Ligi Kuu ilikuwa Agosti 24, 2013 ilipoitwanga Ashanti FC mabao 5-1, shukrani kwa Jerry Tegete, aliyefunga mawili, Simon Msuva, Haruna Niyonzima na Nizar Khalfan, la kufutia machozi la wapinzani wao likiwekwa kimiani na Shaaban Juma, msimu wa 2013/14.

Rekodi inaonyesha katika michezo 11 ambayo timu hizo zimecheza hadi juzi, Yanga imeshinda mara nane, sare mbili na KMC iliyoanza kucheza ligi msimu wa 2018/19 imeshinda mara moja tu.

Ilikuwa ni Machi 12, 2020, Ligi Kuu msimu wa 2019/20 timu hiyo inayomilikiwa na Manispaa ya Kinondoni Dar es Salaam iliposhinda bao 1-0.

Mechi ya juzi ndiyo iliyotoa mabao mengi zaidi, katika mechi zote 10 za nyuma hakuna timu iliyoshinda zaidi ya mabao mawili.

Job anaingia kwenye historia ya timu hiyo kwa kuwa beki wa kwanza kufunga bao la kwanza la msimu kwa timu hiyo kwa zaidi ya misimu 16 iliyopita.

Mabeki, Bakari Mwamnyeto na Kelvin Yondani, wameshafunga mabao katika mechi ya kwanza kwa misimu tofauti katika timu hiyo, lakini yalikuwa ya pili kwenye mchezo na si ya kufungua msimu.

Msimu wa 2018/19 Yondani alifunga bao la pili katika mechi ya ufunguzi dhidi ya Mtibwa la kwanza likifungwa na Herieter Makambo kwenye ushindi wa 2-1, na msimu uliopita Mwamnyeto alifunga bao la pili katika mechi dhidi ya Polisi Tanzania, la kwanza likifungwa na Fiston Mayele, Yanga ikishinda pia mabao 2-1.

# Nyota judo wajifua ughaibuni

**Na Shufaa Lyimo**

WACHEZAJI watatu wa Timu ya Taifa ya judo, Adam Mwakisoma, Edo Thomas na Hemed Said, wameweka kambi nje ya Tanzania kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya kusaka tiketi ya kushiriki Michezo ya Olimpiki itakayofanyika kuanzia Septemba 4 hadi 9, mwaka huu huko Morocco.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Chama cha Judo Tanzania (JATA), Innocent Mallya (pichani), alisema mchezaji mmoja yupo Ufaransa na wenzake wawili wapo Jamhuri ya Azerbaijan.



Mallya alisema wameamua kuwapeleka katika nchi hizo kutokana uhaba wa miundombinu hapa nchini lakini wakiwa huko watapata nafasi ya kutumia vifaa vya kisasa.

"Tunaamini wachezaji wetu wataiwakilisha vizuri Tanzania katika mashindano yajayo kutokana na mazoezi wanayoendelea kufanya," alisema Mallya.

Katibu huyo aliongeza JATA inatarajia kuandaa mashindano ya ndani yatakayofanyika Novemba, mwaka huu yenye lengo la kuibua wachezaji wapya vijana.

Pia ameiomba serikali iwasaidie kuwalipia ushuru ili wafanikiwe kupata vifaa vyao vya michezo ambavyo vimekwama bandarini kutokana na kukosa fedha za kulipa ushuru.




Wachezaji wa Singida Fountain Gate, wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya marudiano ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya JKU ya Zanzibar itakayochezwa keshokutwa. Tayari kikosi hicho kimeshatua Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

## Beki Simba atarajia makubwa Ligi Kuu Bara

**Na Saada Akida**

LICHA ya kutopata nafasi ndani ya kikosi cha kwanza cha Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliviera 'Robertinho', beki wa timu hiyo, Hussein Kazi, amesema hana presha na anaimani ipo siku atapata namba na mashabiki 'wataliimba' jina lake.

Kazi amesajiliwa na Simba akitokea Geita Gold FC kwa lengo la kuongeza nguvu katika safu ya ulinzi ambayo kwa sasa inaongozwa na Henock Inonga na Che Fondoh Malone.



Akizungumza na Nipashe jana, Kazi alisema anaamini muda wake wa kucheza katika kikosi cha kwanza haujafika na anaahidi nafasi hiyo ikipatikana ataonyesha kiwango kuzuri kitakachomshawishi Robertinho.

Kazi alisema kwa sasa anaendelea kujifunza mambo mbalimbali kutoka kwa wachezaji aliowakuta na wenye uzoefu huku akiwaambia mashabiki waendelee kuwa na subira.

"Naamini siku yangu itafika na nitapata namba katika kikosi cha kwanza, hayo ni malengo yangu na ninazidi kujiimarisha, kwa muda mfupi niliokaa hapa nimejifunza mambo mengi katika kujijenga," alisema Kazi.

## Uhamiaji yaanza mawindo mapema

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Uhamiaji inayoshiriki Ligi Kuu Zanzibar imesema imeanza mazoezi mapema kwa ajili ya kujiandaa na msimu mpya ili kufikia malengo yake baada ya msimu uliopita kushindwa kutwaa taji lolote, imeelezwa.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Abdi Salehe, alisema wamefanya usajili mzuri ambao utaendana na ushindani wa Ligi Kuu Zanzibar na kwa misingi hiyo anaamini watatimiza malengo.

Salehe alisema tayari wamesajili wachezaji wapya saba ambao watakiongezea nguvu kikosi chao kuelekea msimu mpya.

"Tumefanya usajili mzuri, tumeridhishwa na viwango vyao kupitia michezo kadhaa ya kirafiki tuliyocheza, tuna matumaini ya kufanikisha malengo ya kutwaa makombe mawili msimu huu, pia tumeacha wachezaji watano," alisema Salehe.

Kocha huyo alisema usajili waliofanya umezingatia changamoto za kiufundi walizokuwa nazo katika nafasi mbalimbali ambazo zilichangia kuwafelisha.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### NUNES ATAJWA CITY

MANCHESTER City inatathmini mpango wa kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Ureno, Matheus Nunes, 24, kutoka Wolves. ***(Athletic)***

### WOLVES KUMUUZA NUNES

KUNA uwezekano mkubwa wa Wolves kumruhusu, Matheus Nunes kuondoka kwenye Uwanja wa Molineux endapo Manchester City watatoa ofa kubwa kwa mchezaji huyo. ***(Express & Star)***

### EZE AINGIA SOKONI

MANCHESTER City pia wameelekeza darubini yao kwa kiungo mshambuliaji wa Crystal Palace na England, Eberechi Eze, mwenye umri wa miaka 25, baada ya kusitisha mpango wao wa kumnunua kiungo wa West Ham na Brazil, Lucas Paqueta (25). ***(Times)***

### FLUMINENSE: ANDRE HAUZWI

KLABU ya Fluminense haitamuuza kiungo Mbrazil, Andre mwenye umri wa miaka 22 mwaka huu licha ya Liverpool, Fulham na Sporting Lisbon kumtaka. ***(O Globo)***

### PEPE KUELEKEA SAUDIA

MSHAMBULIAJI wa Arsenal na Ivory Coast, Nicolas Pepe, mwenye umri wa miaka 28, anatarajiwa kuhamia Saudi Arabia baada ya kukataa nafasi ya kujiunga na Besiktas. ***(RMC kupitia Metro)***

### LUKAKU NJIA MOJA

CHELSEA itamsihi mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 30 kukubali ofa kutoka Saudi Arabia iwapo makubaliano hayawezi kufikiwa na klabu mojawapo ya Ulaya. ***(Talksport)***

### JUVE YAMTAKA LUKAKU

JUVENTUS iko tayari kuilipa Chelsea pauni milioni 35 kwa ajili ya Romelu Lukaku, lakini Waitaliano hao wanasubiria pauni milioni 50 kutokana na mauzo ya mshambuliaji wa Serbia, Dusan Vlahovic (23), kabla ya kuendelea na mpango huo. ***(Standard)***

### LLORIS MAMBO BADO

KLABU ya Lazio imesitisha azma yao ya kumsajili mlinda mlango wa Tottenham Hotspur mwenye umri wa miaka 36, Hugo Lloris. ***(Fabrizio Romano)***

### KUDUS ANUKIA WEST HAM

KLABU ya West Ham bado ipo kwenye mazungumzo na Ajax kuhusu mpango wa kumnunua kiungo wa kati wa Ghana, Mohammed Kudus, mwenye umri wa miaka 23 baada ya ofa mbili kukataliwa. ***(Telegraph)***

### EN-NESYRI KUTUA WEST HAM

WEST Ham pia wameanzisha mazungumzo na Sevilla kuhusu uwezekano wa kumnunua mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Morocco, Youssef En-Nesyri mwenye umri wa miaka 26. ***(Sky Sports)***

### GONZALEZ ANUKIA EPL

BRENTFORD imewasilisha ofa iliyoboreshwa ya kumnunua winga wa Fiorentina, Nico Gonzalez, lakini klabu hiyo ya Serie A na mchezaji huyo wa Hispania mwenye umri wa miaka 21 hawana nia kufanya mazungumzo ya uhamisho. ***(Football Italia)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ARSENAL YAIWEKEA DAU NONO CHELSEA

**LONDON,** England

●●● Ni katika kufanikisha usajili wa mshambuliaji, Balogun ambaye...

CHELSEA bado inamtaka mshambuliaji wa Arsenal, Folarin Balogun, baada ya mazungumzo ya awali na washikabunduki hao, lakini kwa sasa hawako tayari kufikia bei inayotakiwa ya pauni milioni 50, kwa mujibu wa 90min.

**Chelsea wanatafuta mshambuliaji mpya wa kumpunguzia mzigo Nicolas Jackson na wanamlenga zaidi Balogun, ambaye alifunga mabao 21 katika kipindi cha mkopo akiwa na Stade Reims ya Ufaransa msimu uliopita.**

Baada ya kuwasiliana na wawakilishi wa mchezaji huyo wa Arsenal, Chelsea bado wana nia ya kutaka kumnunua mshambuliaji huyo raia wa Marekani ingawa 90min inaelewa The Blues hao hawako tayari kulipa kiasi cha pauni milioni 50 kinachotakiwa.

Hivi karibuni ofa ya Monaco ya pauni milioni 30 kwa Balogun ilikataliwa, huku nia ya mapema ya Inter Milan kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 ilitoweka haraka pale bei ya pauni milioni 50 ilipowekwa.

Chelsea inatarajia kumsajili mshambuliaji mpya kabla ya dirisha la usajili kumalizika na pia wanataka mshambuliaji mpya mahiri ambaye anaweza kusaidia kuziba pengo la Christopher Nkunku, ambaye alicheza kama namba 10 na winga katika mechi za kujiandaa na msimu kabla ya kuumia goti.

Uhamisho wa nyota wa Crystal Palace, Michael Olise ulikuwa karibu kukamilika kabla ya Mfaransa huyo kutia saini mkataba mpya, na kuifanya Chelsea kulazimika kufikiria chaguzi mbadala.

Nia inasalia kwa Mohammed Kudus wa Ajax, ambaye West Ham United imeshindwa katika ofa zake mbili.

Ajax ya Uholanzi inasemekana kushikilia dau la euro milioni 50 na wameonya hadharani wanaomtaka Kudus wataongeza bei wanayotaka wakati tarehe ya mwisho ya kuhama inakaribia.

Chelsea pia wanajulikana wanawataka wachezaji wawili wa Lyon, Rayan Cherki na Bradley Barcola

SHEFFIELD YAINGIA SOKONI

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,146,3

MECHI KALI
CELTA VIGO
VERSUS
REAL MADRID
1 | 4.53
X | 3.84
2 | 1.76

tigo pesa SportPesa
WASHINDI WA MAOKOTO Deilee!
1. Tayana Mmbaga - 0653 727 XXX
2. Hashimu Abrahman - 0654 223 XXX
3. Iddi Saidi - 0659 322 XXX
4. Godwin Mbawala - 0659 411 XXX
5. Lawrance Kontua - 0672 405 XXX
6. Fadhili Manzi - 0674 302 XXX
7. Timotheo Sunza - 0719 210 XXX
8. Bujirima Bujirima - 0769 997 XXX
9. Nicko Twalale - 0673 816 XXX
10. Issah Twanje - 0655 652 XXX
20,000/= KWA KILA MMOJA

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# LIVERPOOL YABANIWA KUMSAJILI ANDRÉ

**LIVERPOOL,** England

LIVERPOOL wametoa ofa ya euro milioni 30 kwa kiungo wa Fluminense, André iliyokataliwa na klabu hiyo ya Brazil, vyanzo vimeithibitishia ESPN Brasil.

Klabu hiyo ya Merseyside inamtaka André ajiunge nao kabla ya dirisha la usajili kufungwa Septemba Mosi, lakini Fluminense wanasita kumruhusu mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil kuondoka kabla ya mwisho wa msimu wao.

Bodi ya Fluminense ilifahamisha Liverpool hata kama wangetoa ofa kwa André hawatamruhusu mchezaji huyo kuondoka kwa sasa.

Liverpool wanahitaji kuimarisha safu yao ya kiungo kufuatia kuondoka kwa Fabinho na Jordan Henderson waliokwenda Saudi Arabia.

Fabinho alijiunga na Al Ittihad kwa uhamisho wa euro milioni 40 tangu Julai 31, mwaka huu huku Henderson akihamia Al Ettifaq kwa dili la euro milioni 14.

Chini ya mkataba na Fluminense hadi Desemba, mwaka 2026, Andre mwenye umri wa miaka 22 ni mchezaji muhimu wa Kocha, Fernando Diniz.

Amecheza mechi 40 za timu hiyo msimu uliopita na amevutia hisia za klabu kadhaa za Ulaya. Fulham walikuwa na ofa ya euro milioni 20 kwa André iliyokataliwa na mapema mwaka huu.

Fluminense wana matumaini makubwa ya kushinda Copa Libertadores (Ligi ya Mabingwa Amerika Kusini) msimu huu.



# Silva azitosa Barca, PSG

**MANCHESTER,** England

BERNADO Silva ameongeza mkataba wa nyongeza katika klabu ya Manchester City, klabu hiyo imetangaza.

Kiungo huyo wa kati wa Ureno ameongeza mkataba wa mwaka mmoja utakaomuweka hapo kwenye Uwanja wa Etihad hadi mwaka, 2026.

Silva amekuwa akihusishwa na kuhamia Barcelona na Paris Saint-Germain msimu huu wa joto, lakini mkataba wake mpya unamaanisha atasalia Manchester baada ya tarehe ya mwisho ya kuhama ambayo ni Septemba Mosi.

"Nimekuwa na miaka sita ya ajabu hapa Manchester City na nina furaha kuongeza muda wangu hapa," alisema Silva.

"Kushinda mataji matatu msimu uliopita lilikuwa jambo la kipekee sana na inafurahisha kuwa sehemu ya kikosi ambacho kina njaa na shauku.

"Mafanikio yanakufa[...] utake zaidi, na Klabu[...] inanipa fursa hiyo ya k[...] delea kushinda.

"Ninampenda ko[...] wachezaji wenzangu[...] mashabiki na natum[...] tunaweza kushiriki kum[...] kumbu kubwa zaidi ka[...] miaka ijayo."

City pia wanaka[...] kutangaza mkataba m[...] kwa Kyle Walker, aml[...] amekuwa akihusishwa[...] kuhamia Bayern Mu[...] msimu huu wa joto.

## HABARI MICHEZO


322,426/-


# AZAM YAJIPANGA KULIPA KISASI KWA WAHABESHI

Na Saada Akida

MATAJIRI wa Chamazi, Azam FC wanatarajia kuivaa Bahir Dar Kenema kutoka Ethiopia katika mechi ya marudiano ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Katika mechi ya kwanza iliyochezwa mjini Bahir Dar wiki iliyopita, Azam ilichapwa mabao 2-1.

**Kuelekea mchezo huo, Kocha Mkuu wa Azam, Youssouph Dabo, alisema amefanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza katika mechi iliyopita na wamejipanga vizuri kutumia uwanja wa nyumbani.**

Dabo alisema anaamini kikosi chake kitapata matokeo chanya ambayo yatawasaidia kusonga mbele katika michuano hiyo na wachezaji wapo tayari kwa mapambano.

Kocha huyo alisema wataingia uwanjani kwa lengo la kulipa kisasi kwa kupata ushindi ambao utawasaidia kusonga mbele katika michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

"Haitakuwa mechi rahisi, tumeona ubora wa wapinzani wetu na madhaifu yao, pia nao wametuona vizuri, kila mmoja wetu anahitaji kupata ushindi, tutacheza kwa nidhamu kubwa na kuwaheshimu ili kupata matokeo mazuri yatakayotuvusha hatua nyingine ," alisema Dabo.

Naye mshambuliaji wa Azam FC, Idriss Mbombo (pichani), amewaita mashabiki wa timu hiyo kujitokeza kwa wingi uwanjani kwa sababu wamejipanga kulipa kisasi.

"Tuko tayari kwa ajili ya kulipa kisasi, tunaamini siku ya kesho (leo) tutawapa furaha mashabiki wetu kwa kuvuka hatua hii na kusonga mbele hadi kucheza makundi," alisema Mbombo.



Watoto kutoka sehemu mbalimbali wakicheza mpira wa magongo katika viwanja vya JKM Park, Dar es Salaam, juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Mabeki waitesa Simba

INATOKA UKURASA 24

kabambe wa kiufundi ili timu yetu isiwe inaruhusu mabao mepesi. Kama litafungwa basi iwe kwa bahati mbaya sana na si mara zote na timu zote hata za kawaida tu," alisema Ahmed.

Akitoa tathmini ya mechi mbili kwa timu yake alisema kikosi kimeanza kupata muunganiko na baada ya muda mfupi wanaamini kitakuwa tishio si dhidi ya timu za Tanzania tu, bali hata katika michuano ya kimataifa.

"Tathmini yangu, sisi tumeridhika, tunaona timu yetu inatoka hatua moja kwenda nyingine, tunaamini timu ikiendelea hivi hivi na wachezaji kuzoeana tutakuwa na timu tishio sana huko mbele, unaona kule mbele wafungaji wameongezeka, straika, Moses Phiri amerejea, tena siyo kurejea tu, amekuja na makali yake.

Tunaona mwanga katika timu yetu na tumeridhika kwa sababu hatujapoteza mechi yoyote mpaka sasa, si kwenye ligi tu bali tangu kuanzia michuano ya Ngao ya Jamii tumeichukua, tuko imara," alisema meneja huyo.

## *Yanga yahamishia*

INATOKA UKURASA 24

na muda wowote anatarajiwa kurejea nchini kuungana na wenzake.

"Kocha amesema ni wakati wa kuwapa nafasi wachezaji ambao hawajawahi kucheza ili kila Mtanzania pamoja na mashabiki waweze kuona viwango vyao," aliongeza Kamwe.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa KMC, Abdihamid Moallini, alikiri wachezaji wake kufanya makosa ambayo yaliwaadhibu na kupelekea kufungwa idadi kubwa ya mabao.

Alisema timu yake haikucheza vizuri na hakutarajia kupata matokeo hayo ambayo yanamrejesha kwenye uwanja wa mazoezi kufanyia kazi mapungufu kwa ajili ya kurejea tena uwanjani wakiwa imara.

"Tunawapongeza wapinzani wetu, tunarejea kwenye uwanja wa mazoezi kurekebisha makosa yetu kwa ajili ya mchezo ujao wa ligi hiyo," alisema Moallini.


SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 26/08/23 | 17:00 | Everton FC vs Wolverhampton Wanderers | 2.26 | 3.25 | 3.05 |
| 02. 26/08/23 | 20:00 | Cadiz CF vs UD Almeria | 2.23 | 3.25 | 3.05 |
| 03. 26/08/23 | 20:00 | SC Farense vs GD Chaves | 2.36 | 3.10 | 3.00 |
| 04. 26/08/23 | 20:30 | Granada CF vs RCD Mallorca | 2.55 | 2.90 | 2.95 |
| 05. 26/08/23 | 21:45 | KV Kortrijk vs Standard Liege | 2.95 | 3.45 | 2.21 |
| 06. 26/08/23 | 22:00 | Excelsior Rotterdam vs Fortuna Sittard | 2.22 | 3.50 | 2.90 |
| 07. 27/08/23 | 02:30 | New York Red Bulls vs Inter Miami CF | 2.40 | 3.30 | 2.50 |
| 08. 27/08/23 | 13:15 | PEC Zwolle vs FC Utrecht | 2.90 | 3.60 | 2.21 |
| 09. 27/08/23 | 16:00 | Strasbourg Alsace vs Toulouse FC | 2.09 | 3.50 | 3.20 |
| 10. 27/08/23 | 16:30 | FSV Mainz vs Eintracht Frankfurt | 2.48 | 3.45 | 2.55 |
| 11. 27/08/23 | 17:00 | St. Truidense VV vs Cercle Brugge | 3.05 | 3.30 | 2.23 |
| 12. 27/08/23 | 17:00 | St Mirren FC vs Aberdeen FC | 2.41 | 3.20 | 2.85 |
| 13. 27/08/23 | 17:30 | Boavista Porto vs Casa Pia Lisbon | 2.22 | 3.15 | 3.20 |
| 14. 27/08/23 | 17:45 | SC Heerenveen vs Sparta Rotterdam | 2.26 | 3.50 | 2.85 |
| 15. 27/08/23 | 18:00 | Racing Club de Ferrol vs Sporting Gijon | 2.31 | 3.00 | 3.20 |
| 16. 27/08/23 | 18:00 | Sandefjord Fotball vs FK Haugesund | 2.21 | 3.20 | 2.80 |
| 17. 27/08/23 | 18:30 | Newcastle United vs Liverpool FC | 2.11 | 3.75 | 2.95 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 25/08/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 3495 | Dewa United vs Persija Jakarta | 2.95 | 3.25 | 2.10 |
| 16:30 | 3021 | Shabab AL Sahel vs Safa SC | 1.64 | 3.51 | 4.88 |
| 17:00 | 1042 | Emirates Club vs Ajman Club | 3.23 | 3.54 | 1.93 |
| 17:00 | 1934 | FC Olimpik vs FK Turon | 1.67 | 3.40 | 4.40 |
| 17:30 | 4515 | Gazovik Orenburg vs CSKA Moscow | 3.60 | 3.81 | 1.82 |
| 18:50 | 5929 | AL Qadsia vs Khaitan SC | 1.50 | 4.13 | 4.94 |
| 19:00 | 4101 | Pribram vs Dukla Prague | 3.38 | 3.43 | 1.92 |
| 19:10 | 2168 | SKN St Polten vs Floridsdorfer AC | 1.95 | 3.56 | 3.26 |
| 19:10 | 3549 | DSV Leoben vs First Vienna | 1.82 | 3.71 | 3.56 |
| 19:30 | 1033 | Radnicki Nis vs FK Radnicki 1923 | 1.96 | 3.13 | 3.58 |
| 19:30 | 3089 | Paderborn vs Kaiserslautern | 1.97 | 3.76 | 3.26 |
| 19:30 | 4459 | Randers vs Viborg FF | 2.92 | 3.52 | 2.23 |
| 19:30 | 4863 | Schalke 04 vs Holstein Kiel | 1.82 | 3.95 | 3.60 |
| 20:00 | 2895 | Fakel vs FC Krasnodar | 3.50 | 3.39 | 1.96 |
| 20:00 | 3983 | Horsens vs Naestved BK | 1.62 | 3.99 | 4.14 |
| 20:30 | 1450 | Red Star vs Sochaux | 2.03 | 3.31 | 3.46 |
| 20:30 | 1891 | Cholet vs Nancy | 2.12 | 3.34 | 3.19 |
| 20:30 | 2213 | Al Rayyan SC vs Qatar SC | 1.96 | 3.58 | 3.13 |
| 20:30 | 4333 | Las Palmas UD vs Real Sociedad | 4.06 | 3.18 | 2.04 |
| 20:30 | 4389 | Nimes vs Le Mans | 2.09 | 3.30 | 3.30 |
| 20:30 | 5618 | Ajax Cape Town vs Chippa Utd | 2.20 | 2.83 | 3.55 |
| 20:30 | 5691 | Stade Nyonnais vs FC Sion | 3.77 | 3.52 | 1.78 |
| 21:00 | 1012 | Den Bosch vs ADO Den Haag | 3.02 | 3.38 | 2.13 |
| 21:00 | 1129 | FC Eindhoven vs NAC Breda | 2.40 | 3.38 | 2.61 |
| 21:00 | 1880 | VVV Venlo vs Jong Utrecht | 1.47 | 4.29 | 5.51 |
| 21:00 | 1966 | Dordrecht vs Maastricht | 2.52 | 3.49 | 2.43 |
| 21:00 | 3410 | Al Fateh (KSA) vs Al Nasr Riyadh | 5.33 | 4.34 | 1.53 |
| 21:00 | 4463 | Panetolikos vs PAS Giannina | 2.41 | 3.03 | 3.03 |
| 21:00 | 4468 | HNK Gorica vs Slaven Belupo | 1.73 | 3.44 | 4.15 |
| 21:00 | 5685 | Konyaspor vs Gaziantep BB | 1.69 | 3.81 | 4.33 |
| 21:00 | 5755 | Cambuur vs Jong Ajax | 1.43 | 4.52 | 5.75 |
| 21:00 | 5841 | RFC Seraing vs Zulte Waregem | 2.71 | 3.40 | 2.32 |
| 21:30 | 1318 | Zemplin Michalovce vs FC KoÅice | 2.67 | 3.17 | 2.38 |
| 21:30 | 1928 | U Craiova SA vs Rapid Bucuresti | 2.73 | 3.19 | 2.44 |
| 21:30 | 2300 | Sampdoria vs Pisa | 1.79 | 3.34 | 4.32 |
| 21:30 | 3303 | Dornbirn vs SC Bregenz | 2.27 | 3.53 | 2.66 |
| 21:30 | 4225 | RB Leipzig vs Stuttgart | 1.56 | 4.36 | 5.63 |
| 21:30 | 5316 | Hull City vs Bristol City | 2.31 | 3.23 | 2.88 |
| 21:45 | 1820 | UCD Dublin vs St Patricks | 15.12 | 6.65 | 1.12 |
| 21:45 | 2235 | Bohemians FC vs Derry City | 2.48 | 3.02 | 2.67 |
| 21:45 | 3913 | Shamrock Rovers vs Dundalk FC | 1.61 | 3.58 | 4.74 |
| 21:45 | 4138 | Drogheda Utd vs Cork City | 1.86 | 3.28 | 3.74 |
| 22:00 | 2278 | Nantes vs Monaco | 4.12 | 3.91 | 1.81 |
| 22:00 | 2705 | Chelsea vs Luton Town | 1.29 | 5.59 | 10.26 |
| 22:15 | 3069 | CF Estrela vs GD Estoril | 2.70 | 3.10 | 2.55 |
| 22:15 | 3543 | Grotta vs Throttur Reykjavik | 1.89 | 3.84 | 3.13 |
| 22:30 | 2646 | Audax Italiano vs Coquimbo | 1.98 | 3.31 | 3.41 |
| 22:30 | 5427 | FC Cartagena vs Levante | 2.68 | 3.03 | 2.58 |
| 22:30 | 5579 | Celta Vigo vs Real Madrid | 4.53 | 3.84 | 1.76 |
| 22:45 | 1346 | Varzim vs Lusitania | 1.89 | 3.26 | 3.77 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Ijumaa Agosti 25, 2023

Nipashe



Liver yabaniwa kwa André

UKURASA 22




Kiungo wa Yanga, Pacome Zouzoua (katikati) akijiandaa kuwatoka nyota wa KMC katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam juzi usiku. Yanga ilishinda mabao 5-0. **PICHA: MTANDAO**

## Mabeki waitesa Simba SC Bara

**Na Adam Fungamwango**

ILI kufikia malengo, benchi la ufundi la Simba limeandaa mazoezi maalumu kwa mabeki wake ili kuhakikisha hawaruhusu mabao kirahisi katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika wanayoshiriki, imeelezwa.

Simba imesema itatumia mapumziko ya kalenda ya kimataifa kuimarisha safu yake ya ulinzi.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, amesema moja ya mikakati ya wanayoifanyia kazi ni kuwapa mbinu mpya itakayowasaidia kuzuia kufungwa mabao mepesi kama ilivyotokea walipokutana na Mtibwa Sugar katika mechi ya kwanza ya Ligi Kuu Bara.

"Ile haikuwa nzuri kwa timu kama ya Simba, hii ni timu kubwa, unajua timu yetu hata tukishinda mabao 10, lakini wanachama na mashabiki wetu na hata sisi viongozi huwa tunaumia tukiruhusu hata bao moja hatupendi sana kuruhusu mabao.

Ndio maana tunawekeza sana kutafuta mabeki imara na wazuri, kuimarisha safu yetu ya magolikipa kwa sababu hatupendi hali hiyo," alisema Ahmed.

Alisema tayari matunda yameshaanza kuonekana kwa kulinda lango lao katika mechi ya pili walipowakaribisha Dodoma Jiji mabao 2-0, mechi ikichezwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

"Makocha wanaendelea na mkakati

INAENDELEA UKURASA 23

# Yanga yahamishia majeshi CAF

## Gamondi afurahia 'pacha', kicheko chatawala...

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

WAKATI viungo watatu wa Yanga, Khalid Aucho, Mudathir Yahya na Stephane Aziz Ki wanaonekana kutengeneza 'pacha matata' inayowapatia ushindi, uongozi wa timu hiyo umesema sasa wanaelekeza nguvu kuhakikisha wanafanya vizuri katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

**Nyota hao walionyesha kiwango bora wakati wakipata ushindi wa mabao 5-0 katika mchezo wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya KMC FC uliochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam juzi usiku.**

Yanga inatarajia kuwakaribisha ASAS Djibouti FC katika mechi ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa kesho hapa nchini.

Wachezaji hao watatu katika nafasi hiyo ya kiungo, walionekana kuelewana vyema kiasi cha kumfanya Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, kutamka wazi 'anao vijana' wanaoijua shughuli katikati ya uwanja.

Gamondi alisema viungo hao walianza kuonyesha uelewano kuanzia katika michuano ya Ngao ya Jamii ambapo walipata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Azam FC.

Kocha huyo aliendelea kusema licha ya kupoteza mechi ya fainali, bado kiwango cha Mudathir, Aziz Ki na Aucho kilikuwa bora na kilisaidia kutengeneza mashambulizi dhidi ya wapinzani wao.

Aliendelea kusema viungo hao wameendelea kufanya vizuri walipowavaa ASAS FC katika mchezo wa awali wa Ligi ya Mabingwa Afrika uliochezwa wiki iliyopita kwa kuondoka na ushindi wa mabao 2-0.

Kuhusu mchezo dhidi ya KMC, Gamondi alisema ushindi mnono waliopata umetokana na namna wachezaji wake walivyojituma na kutekeleza yote waliyoambiwa kwenye uwanja wa mazoezi.

"Nimefurahishwa na namna walivyocheza, walijituma sana, ninatarajia wachezaji hawa watakuwa chachu ya mafanikio msimu huu. Mechi ilikuwa nzuri, ninawapongeza wachezaji kwa namna walivyopambana, ule ndio mchezo ninaotaka kuona katika timu yangu katika michezo yote iliyopo mbele yetu hadi mwisho wa msimu.

Tumekuwa tukifanya mazoezi makali ili kuiweka Yanga katika kiwango kizuri na kuwapa furaha mashabiki na leo (juzi) wamefurahi kuona tumetawala mchezo na kupata ushindi mzuri. Bado mimi na wenzangu tunaisuka Yanga ili iwe ile tunayofikiria, tutaendelea kufanyia kazi makosa ya kila baada ya mechi ili tuwe bora zaidi," Gamondi alisema.

Meneja Habari na Mawasiliano wa timu hiyo, Ali Kamwe, alisema klabu inawataka watu wanaojihusisha na uuzaji wa tiketi feki kuacha kwa sababu wakikamatwa itawagharimu.

Kamwe alisema wamekuwa wakipata malalamiko mengi kutoka kwa mashabiki wao wakilalamikia kuuziwa tiketi feki.

"Mara nyingi tnapokea malalamiko kutoka kwa mashabiki wetu wakilalamikia tabia ya watu kuwauzia tiketi feki, kwa yoyote atakayebainika tutamchukulia hatua kali kwa sababu anahujumu uchumi wa nchi yetu," alisema Kamwe.

Meneja huyo alisema pia maandalizi yao kuelekea mchezo wa dhidi ya ASAS yamekamilika na hakuna mchezaji yeyote ambaye ni majeruhi baada ya kumaliza mechi dhidi ya KMC.

Kamwe alisema hali ya kiungo, Mahlatse Makudubela 'Skudu' inaendelea vizuri

INAENDELEA UKURASA 23

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042